# Nipashe

Alhamisi Mei 16, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579919

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13



## Prof. Kabudi azidi ng'anganiwa madai kuishauri vibaya serikali

UKURASA 3




# Biashara 16,000 zafungwa miezi 10

- **Waziri** akiri lakini asema uchumi bado uko imara, awatoa hofu wabunge kwamba watulie... *Endelea ukurasa wa 2*





Maofisa wa polisi wakikagua ajali ya basi la abiria la Mtei Express, linalofanya safari zake kati ya Babati –Dodoma, lenye namba za usajili T 299 AXP, baada ya kugongana uso kwa uso na gari la wanafunzi aina ya Nisani namba za usajili T 390 BHZ (picha ndogo), katika eneo la Himiti, wilayani Babati, Mkoa wa Manyara jana, mwanafunzi wa awali, katika Shule ya Silva Lifu, Osligi Emanuel (3), alifariki dunia papo hapo. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Mbunge CCM alia tozo za trafiki

UKURASA 2

## Mtoto wa miaka mitano akutwa malipo korosho



UKURASA 2

**MICHEZO** **AUSSEMS AFUNGUKA ANAPOIHOFIA MTIBWA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mbunge CCM alia na tozo za trafiki

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Ulanga Mashariki, Godluck Mlinga (CCM), ametahadharisha kutokea kwa mgomo wa madereva wa mabasi nchi nzima kutokana na kile alichokiita uonevu dhidi yao unaofanywa na Jeshi la Polisi na mamlaka nyingine za serikali.

Muda mfupi baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali' bungeni jijini Dodoma jana, Mlinga alisimama na kuomba kuahirisha shughuli za Bunge za jana ili kujadili hoja hiyo ya dharura.

"Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 47 inayotaka kusitisha shughuli za Bunge na kujadili hoja ya dharura. Hivi ninavyoongea, kuna mgomo baridi wa madereva wa mabasi kote nchini ukianzia Morogoro.

"Kwanini madereva wa mabasi wanataka kugoma? Sasa hivi, kwenye mabasi yote kumefungwa ving'amuzi vya VTS na kudhibitiwa na Sumatra na wakizidisha 'speed' 85, wanapata alama moja kwa kila tendo la kuzidisha.

"Kwa mfano kutoka Morogoro hadi Dar es Saalaam kuna umbali wa kilometa 193. Kuna vibao vya 50 vinavyozidi 22. Kuna zebra zinazozidi 22. Ukifuata taratibu zote kutoka Dar es Salaam, kufika Morogoro utatumia muda wa saa sita.

"Mheshimiwa Naibu Spika, ukizidisha 'speed' 50, unapigwa faini na trafiki. Usiposimama kwenye zebra, unapigwa faini na trafiki. Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tendo moja la kuzidisha 'speed' 85 unapopewa alama, jumla ya alama utakazopata kutoka Morogoro hadi Dar es Salaam unaweza kupigwa faini kati ya Sh. milioni mbili hadi tatu kwa safari moja.

"Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wizi, uonevu, tunataka kwenda kwenye nchi yenye uchumi wa kati lakini kwa mwendo huu hatuwezi kufika. Kutokana na hilo, naomba shughuli za Bunge ziahirishwe tujadili hoja hii. Naomba kutoa hoja," Mlinga aliwasilisha.

Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, aliyekuwa anaongoza kikao, alikataa kuahirisha shughuli za jana za Bunge kujadili hoja hiyo lakini akaitaka Serikali kukaa na pande zinazohusika kutatua changamoto zinazolalamikiwa na madereva.

"Kanuni ya 47 inafanya kazi pamoja na Kanuni ya 48. Kwa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Mlinga na kwa mujibu wa Kanuni ya 47(4) na Kanuni ya 48(4), jambo hili linaweza kushughulikiwa katika utaratibu wa kawaida.

"Na kwa sababu baadhi yetu tumelisikia hapa na serikali ipo hapa bungeni, ichukue hatua kuona ni mambo gani ambayo yanalalamikiwa na madereva ili nchi iweze kuendelea wakati huo huo kama waheshimiwa wabunge tukijitahadharisha na ajali zinazotokea.

"Kwa hiyo, upande wa serikali wakutane na hawa madereva kuona shida iko wapi na wamiliki wa vyombo ili wote tuweze kwenda kwa pamoja wakati huo huo wajibu wa serikali kutulinda dhidi ya ajali upo palepale," Dk Tulia aliagiza.

# Biashara 16,000 zafungwa miezi 10

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imesema uchumi wa Tanzania bado uko imara licha ya biashara 16,252 kufungwa katika miezi 10 iliyopita ya mwaka huu wa fedha.

Imelieleza Bunge kuwa madai kwamba uchumi wa nchi umeyumba kutokana na idadi kubwa ya biashara kufungwa si sahihi.

Akichangia mjadala wa makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka ujao wa fedha bungeni jijini Dodoma, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashantu Kijaji, alijibu baadhi ya hoja zilizotolewa na wabunge na kuelekezwa wizarani kwake, akieleza kuwa takwimu za serikali zinaonyesha biashara zinazofungwa ni chache kuinganisha na zinazofunguliwa.

"Sina sababu ya kudanganya kwa sababu muda wote niko 'field', biashara zilizofungwa na zilizofunguliwa tunazijua. Kuanzia Julai mwaka jana hadi Aprili mwaka huu, biashara zilizofungwa zilikuwa 16,252 na zilizofunguliwa ni 147,818.

"Huo ndio ukweli, kama biashara zimefungwa TRA (Mamlaka ya Mapato) ingewezaje kukusanya kodi? Kama hali ingekuwa hivyo, Tanzania ingekuwa na 'dormant economy' (uchumi uliolala).

"Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi uko imara, uko makini na tunaendelea kutenda kwa ajili ya Watanzania, ndiyo maana tangu Mheshimiwa Rais (John) Magufuli aingie madarakani, hatujawahi kushuka chini ya Sh. trilioni moja kukusanya kodi kila mwezi, huo ndiyo uhalisia tunaoujua," Dk. Kijaji alisema.

Naibu waziri huyo pia alizungumzia suala la kukwama kwa mafuta ya kula bandarini, akieleza kuwa uhalali wa mzigo unapaswa kuthibitishwa na mwagizaji mwenyewe.

"Tunachokifanya ni kufuata taratibu, Watanzania halali wamemwelewa Rais Dk. John Magufuli. Mwaka jana, ombwe kama hili la mafuta lilitokea, lakini lazima tujiulize, kwanini huwa 'wana-target' kipindi hiki cha Mfungo wa Ramadhani?

"Sheria inasema hiki ni chakula, tuonyeshe unatuletea kutoka nchi gani? Kwa 'original documents' (nyaraka halisi) tunataka Watanzania walindwe," alisema.

Dk. Ashantu aliongeza kuwa hadi sasa, metriki tani 14,400 za mafuta ya kupikia, nyaraka zake hazijawasilishwa.

"Mafuta hayo yapo, mengine walisema yanatumika nje ya nchi, lakini waliyatoa na kuyaingiza ndani," Dk. Ashatu alisema.

**VIWANDA VYA KOROSHO**

Naibu Waziri wa Kilimo, Omar Mgumba, alisema msimu ujao, korosho nyingi zitabanguliwa nchini kutokana na wawekezaji wengi kujitokeza kujenga viwanda vya kubangua korosho. Alisema kangomba ni ujasiriamali ambao sasa unapaswa

INAENDELEA UK. 8



Rais Dk. John Pombe Magufuli na mkewe Mama Janeth Magufuli, wakitoa heshima za mwisho kwa mwili wa marehemu Festo Rutamigwa Isokoza, katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, jijini Dar es Salaam jana. Marehemu enzi za uhai wake, alikuwa mtaalamu wa kilimo alifanya kazi JWTZ na taasisi zake, kabla ya kustaafu na alikuwa rafiki mkubwa wa Rais Magufuli ambaye walisoma pamoja tokea darasa la kwanza hadi la saba katika Shule ya Msingi ya Chato, mkoani Geita na baadaye elimu ya sekondari katika seminari ya Katoke, Biharamulo mkoani Kagera. **PICHA: IKULU**

# Mtoto wa miaka 5 akutwa malipo ya korosho

**Na Lucy Ogutu,** MTWARA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Mtwara, imewafikisha mahakamani watuhumiwa wawili akiwamo mfanyakazi wa benki ya NMB Wilaya ya Nanyumbu kwa kuingiza jina la mtoto mwenye umri wa miaka mitano katika malipo ya korosho.

Watuhumiwa hao wanashtakiwa kwa makosa ya kugushi na utakatishaji wa fedha.

Wanadaiwa kwa udanganyifu huo kujipatia Sh. milioni tano kinyume na sheria za nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Mtwara, Stephen Mafipa, alisema watuhumiwa hao ni Juma Mbevu, ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Ushirika cha Napacho Amcos na Agustino Nziku, ambaye ni mfanyakazi wa benki ya NMB, Wilaya ya Nanyumbu, ambao ilidaiwa kuwa walishirikiana kufanya kosa hilo.

Alisema watuhumiwa kwa pamoja wanashtakiwa kwa makosa ya kula njama, kutenda makosa na kutumia nyaraka zenye maelezo ya uongo kumdanganya mwajiri kinyume na vifungu namba 32 na 22 vya Sheria ya Kuzuia na kupambana na rushwa.

Alisema jina la mtoto wa mtuhumiwa Augustino Nziku, ambaye ni mfanyakazi wa benki ya NMB, Wilaya ya Nanyumbu liliingiziwa kwenye orodha ya malipo huku wakijua mtoto huyo hastahili kuuza korosho hivyo kumwezesha mtuhumiwa kujipatia kiasi cha Sh. milioni tano ambazo hakustahili.

Kesi hiyo ya uhujumu uchumi imefunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara, eneo ambalo watuhumiwa walitenda kosa hilo.

Alisema kesi zingine za udanganyifu katika malipo ya korosho bado zinaendelea kuchunguzwa na zikikamilika wahusika watafikishwa katika vyombo vya sheria.

HABARI KITAIFA

# JPM amtumbua Makalla Katavi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, ametengua uteuzi wa Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Amos Makalla.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, Rais Magufuli amemteua Juma Homera kuwa Mkuu wa Mkoa huo kuanzia juzi.

Taarifa hiyo ilisema kuwa kabla ya uteuzi huo, Homera alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Tunduru Mkoa wa Ruvuma.

"Homera anachukua nafasi ya Makalla ambaye uteuzi wake umetenguliwa, uteuzi wa Homera unaanza Mei 14," ilieleza taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilisema uteuzi wa Mkuu wa Wilaya ya Tunduru utafanywa baadaye.

**JPM ALIVYOMMWAGIA SIFA**

Alipokuwa kwenye ziara mkoani Ruvuma hivi karibuni, Rais Magufuli alimpongeza Mkuu wa Wilaya hiyo, Homera kuwa amekuwa mkali na amesimama vyema kusukuma maendeleo.

"Inawezekana hamumhitaji sana hapa, lakini kama kuna mikoa itakuwa imezubaa zubaa mtu nitakayempa ukuu wa mkoa ni huyu hapa (Homera), anajua kunyoosha mambo mimi sisemagi pembeni" alisema na kuongeza:

"Najua makangomba wanamchukia, unataka kupendwa na wote umeshapendwa na mke wako imeshatosha, hata angefanyaje hawezi kupendwa na wote, kwa hiyo wewe chapa kazi," alisema Rais Magufuli wakati huo.

**MAKALLA NI NANI?**

Makalla aliteuliwa kwa mara ya kwanza kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Rais mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, Septemba 14, 2015.

Machi 12, 2016, wakati Rais Magufuli alipofanya uteuzi wa wakuu wa mikoa wapya alimhamishia Makalla Mkoa wa Mbeya kabla ya kumpeleka Katavi Julai, mwaka jana.

Makalla pia aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwenye serikali ya Kikwete na baadaye Mweka Hazina wa CCM Taifa.

Makalla aliingia bungeni kwa mara ya kwanza mwaka 2010 kupitia Jimbo la Mvomero akimwangusha kwenye kura za maoni aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo (CCM), Suleman Sadiq.

Kwa mara ya kwanza, Makalla alianza kuwania jimbo hilo mwaka 2005 lakini aliangushwa na Murad kwa kura chache kwenye kura za maoni ndani ya chama hicho.

Makalla pia aliwahi kuwa Mweka Hazina wa CCM, Taifa na Kaimu Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) na nafasi zingine kwenye umoja huo.




Mkuu wa wilaya ya Temeke, Felix Lyaniva (kushoto), akikabidhi bendera ya taifa kwa washiriki watatu, Mohammad Faiz (kulia) na wenzake, Shamsuddin Hussen (katikati)na Sumayya Juma (wa tatu kulia) jijini Dar es Salaam jana, kwaajili kuiwakilisha nchi katika mashindano makubwa ya usomaji wa Qur-aan Afrika 2019, yatakayofanyika kesho kutwa katika Uwanja wa Taifa jijini. Wengine ni baadhi ya viongozi wa mashindano hayo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wabunge wazidi kumbana Prof. Kabudi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BAADHI ya wabunge wameendelea kumtaka Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, kujiuzuu ili kuonyesha kuwajibika kutokana na kile walichokiita ushauri wake mbovu kwa serikali.

Hoja ya kumtaka Prof. Kabudi kujiuzulu ilitolewa juzi bungeni na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iipowasilisha hotuba yake kuhusu makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka ujao wa fedha.

Kambi hiyo iliwataka Prof. Kabudi, Mawaziri wa Viwanda, Biashara na Wizara ya Kilimo na maofisa wote walioshiriki kutia saini makubaliano ya serikali na Kampuni ya Indo Power ya Kenya kwa ajili ya ununuzi wa korosho, kujiuzulu kutokana na uamuzi wao huo kuisababishia serikali hasara ya Sh. trilioni 1.18.

Akichangia mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara hiyo jana, Mbunge wa Moshi Vijijini, Anthony Komu (Chadema), aliendeleza hoja hiyo akimtaka Prof. Kabudi kujiuzulu kwa kuwa ameitia hasara serikali.

Komu ambaye pia ni Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara, alisema Prof. Kabudi ndiye anapaswa kuwa mtu wa kwanza wa serikali aliyeshuhudia kutiwa saini kwa makubaliano ya serikali na kampuni hiyo ya Kenya, kujiuzulu kwa uamuzi wake umekuwa mara nyingi ukisababisha shida kwa taifa.

Kabla ya kuhamishiwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Kabudi alikuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

"Prof. Kabudi ndiye tatizo kwa nchi hii, ameliingiza taifa hili kwenye matatizo makubwa. Kwa mfano, kwenye korosho, Sheria ya Takwimu, Mpango wa PPP (Ubia wa pamoja katika ya sekta ya umma na binafsi), makinikia na mingine mingi tu," Komu alisema.

Mbunge huyo alilishauri Bunge kuchukua hatua za kumwajibisha waziri huyo kwa kile alichoeleza kuwa amekuwa akifanya uamuzi mbovu na kuwadanganya Watanzania.

Alisema licha ya hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni jana kuwataka Waziri wa Kilimo na Waziri wa Viwanda na Biashara kujiuzulu, yeye anaona waziri wa kujiuzulu kwa sasa ni Prof. Kabudi, akidai wawili hao (Japhet Hasunga na Joseph Kakunda) "wapo ndani ya basi tu, lakini hawajui kinachoendelea."

Hoja hiyo ya kumtaka Prof. Kabudi kuwajibika, pia iliungwa mkono na Mbunge wa Tandahimba, Ahmed Katani (CUF), ambaye alisema kampuni hiyo ya Kenya ililenga kuwatapeli wakulima wa korosho.

Awali akichangia mjadala huo, Mbunge wa Siha, Dk. Godwin Mollel (CCM), alisema serikali haipaswi kupuuza malalamiko ya wabunge, akieleza kuwa ni vigumu kuwekeza nchini kama gharama ya umeme zitaendelea kuwa juu.

"Kwa kuliona hilo, ndiyo maana Rais Magufuli ameamua kuwekeza katika mradi wa umeme wa Stiegler's Gorge. Nilipokuwa kule (upinzani), nilihama na kauli yangu kuungana na wazalendo, kulinda maslahi ya taifa," alisema.

# Bilionea amkana mwanawe kisa mali

**Na Mary Geofrey**

MFANYABIASHARA mkubwa nchini na mmoja wa wanahisa wa kundi la Kampuni za Motisun, Ramanlal Motibhal Patel, amemkana mtoto wake wa pekee, Veer Ramanial Patel, kwa kile alichodai ni kumdhalilisha kwa kuuaminisha umma kuwa ana ugonjwa wa akili.

Katika tangazo lilitolewa na Patel jana kwenye gazeti moja la kila siku, alisema hamtambui mtoto wake wala hahusiki na kitu chochote, hivyo hatawajibika wala kuhusika na wakopeshaji binafsi, benki, wauzaji na wasambazaji wote wanaofanya biashara ya Motisun Group.

"Napenda kuuarifu umma kuwa kuanzia sasa Veer Ramanlal Patel, si mtoto wangu tena wala msimamizi au mdhamini wangu na hausiki na hatahusika na mali zangu zote na masiha yangu nikiwa hai, nitakapokuwa nimekufa, yeye pamoja na mke wake kwa kuwa mimi si baba yake tena," alisema Patel.

Akizelezea chanzo cha kumkana kijana wake huyo, Patel, alisema Januari 30, mwaka huu saa 10:30 jioni alipokea notisi za mikutano 35 ya kampuni za Motisun Group ambao ungefanyika Februari Mosi, mwaka huu.

Alisema mkutano huo, ulikuwa na ajenda kuu ya kila notisi ya kumtoa kwenye ukurugenzi wa kampuni zote 35.

Alisema sambamba na hilo, Januari 31, mwaka huu, mtoto wake wa kiume, Veer, kwa nia ovu, alimwomba kupata uamuzi wa Mahakama ya Wilaya Ilala wa kumpeleka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Kitengo cha Afya ya Akili ili afanyiwe uchunguzi kwa nia ya kuchukua nafasi yake ya ukurugenzi wa kampuni hizo.

Kwa mujibu wa Patel, lengo la kijana wake huyo ni kutaka kumiliki kampuni hizo kwa kigezo kuwa baba yake ana matatizo ya akili, hivyo hawezi kufanya tena biashara.

"Baada ya uchunguzi wa kina wa madaktari bingwa wa Muhimbili ilibainika kwamba nina akili timamu na sina tatizo la afya ya akili. Wakati nikiwa hospitali kwa siku 17 nilitolewa kwenye nafasi yangu ya ukurugenzi wa kampuni zote na nafasi yangu kuchukuliwa na Veer ili kukamilisha dhamira yao ovu," alisema.

Alisema kutokana na mambo yote aliyofanyiwa, amelazimika kumkana mtoto wake huyo na kwamba hatahusika na kitu chake chochote akiwa hai au endapo atafariki dunia.

Taarifa iliyotolewa jana na mmoja wa watu wa familia hiyo, ilikiri kuwa Ramanlal Patel alikuwa akiugua macho kwa muda mrefu na kumsababisha kutoingia ofisini na kutosimamia miradi, hali inayosababisha kazi zote wafanye viongozi wengine.

Kampuni hiyo na bodi iliamua kufanya vikao na kutokana na hali yake hiyo, Mzee Ramanlal apumzike kwenye nafasi ya ukurugenzi na abaki na nafasi ya mmiliki wa hisa ili mtoto Veer achukue nafasi ili kampuni iendelee.

Inadaiwa kuwa baada ya taarifa hizo kuvuja, mmoja wa wapambe wake aliungana na wanasheria hao kumshawishi Patel kukataa ombi hilo.

## KESI YA MBOWE:

# Shahidi adai alipigwa jiwe na kupoteza fahamu

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa tatu, Koplo Rahimu Ramadhani, katika kesi ya uchochezi inayomkabili Mwenyekiti Taifa wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na wenzake wanane, amedai mahakamani siku ya tukio alipigwa jiwe shingoni na kumsababishia kupoteza fahamu wakati akiwazuia waandamanaji wa chama hicho.

Kadhalika alidai kuwa maandamano hayo yaliongozwa na Mbowe, Halima Mdee na washtakiwa wengine watano ambao hawafahamu majina yao.

Koplo Ramadhani alitoa madai hayo jana wakati akitoa ushahidi wake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini cha Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Upande wa Jamhuri uliongozwa Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Paul Kadushi na Mawakili wa Serikali, Wankyo Simon na Jackline Nyantori.

Akiongozwa na Wankyo, shahidi huyo alidai kuwa Februari 16, 2018 aliingia kazini saa 12:00 asubuhi na kituo chake cha kazi ni Oysterbay, jijini Dar es Salaam.

Alidai kuwa aliingia kazini na kupangwa doria mahali tofauti katika mkoa huo wa kipolisi.

"Kati ya saa 11 na 11:15, alasiri tukiwa eneo la Mwenge mimi na makostebo wanne na afande wetu Inspekta Mohammed Mzelengi tulisimama barabara ya ITV tukijadili tuelekee wapi kuendelea na kazi," alidai na kuongeza:

"Kupitia redio upepo tulipokea maelekezo kutoka kwa afande Dotto akitutaka tuelekee katika viunga vya Buibui kuongeza nguvu ya ulinzi, tulipofika eneo hilo nilimwona Mbowe akimnyang'anya kipaza sauti mgombea akitoa maelekezo kuwashinikiza viongozi wenzake kufanya maandamano," alidai Koplo Ramadhani.

Alidai kuwa alisikia wananchi wakiitikia maelekezo kwamba 'lazima tuandamane kwenda kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni' alinukuu shahidi.

Koplo Msangi alidai, mbowe baada ya kuwatangazia wanachama wake waandamane, alishuka chini na kushikana mikono na viongozi wenzake waliokuwapo eneo hilo na kuandamana wakipitia barabara ya Mwananyamala, Kinondoni Studio hadi Kawawa.

Alidai kuwa wandamanaji walikuwa wameshika mawe, marungu na chupa za maji na walipofika eneo la Mkwajuni, polisi walitoa ilani ya kuwataka watawanyike, lakini walikaidi.

Alidai, waandamanaji hao waliwarushia polisi mawe na marungu na yeye alipigwa jiwe eneo la shingoni na baada ya hapo hakufahamu kilichoendelea na kujikuta yupo hospitali amelazwa.

Alidai alilazwa katika hospitali ya polisi iliyopo Barabara ya Kilwa na aliposhtuka alikumbuka kwamba alikuwa na silaha aina ya SMG ambayo wakati huo hakuwa nayo.

Alidai kuwa kesho yake alimwuliza bosi wake kuhusu silaha yake akafahamishwa kwamba ilirejeshwa Kituo cha Polisi Oysterbay.

Wakili wa utetezi, Peter Kibatala alimhoji kama ifuatavyo:

**Kibatala:** Shahidi utaratibu wa Jeshi la Polisi ukoje askari anapokabidhiwa silaha anaruhusiwa mtu mwingine kuirejesha?

**Shahidi:** inategemea na mazingira ya askari.

**Kibatala:** Ieleze mahakama kama inaruhusiwa au hairuhusiwi?

**Shahidi:** Inawezekana kurudishwa na mtu mwingine inategemea na mazingira ya mhusika.

Mbali ya Mbowe, washtakiwa wengine ni, Mbunge wa Bunda Ester Bulaya, Mbunge wa Tarime Mjini Esther Matiko, Katibu Mkuu Taifa,

INAENDELEA UK. 8



Mkazi wa jiji akijaribisha koti la mtumba, kabla ya kulinunua kando ya Barabara ya Uhuru, eneo la Ilala TBL, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Jafo awaonya wakuu wa mikoa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amewataka wakuu wa mikoa kutumia uongozi wao vizuri ili kujiepusha kusababisha madhara kwa kiongozi mkubwa wa nchi.

Jafo alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizungumza na wakuu wa mikoa katika kikao cha tathmini ya utoaji wa vitambulisho kwa wajasiriamali nchini.

Alisema huwa inampa tabu kiongozi anapowadhalilisha watumishi wa umma kwa kiwango kikubwa.

"Naomba muende kulifanyia kazi, sisi sote ni viongozi hakuna mkamilifu hata Mungu anatufahamu, nendeni mkabadilike ili kupata hamasa kwa watumishi na mabadiliko makubwa," alisema.

Aliwataka wawafanye watumishi waliochini yao kuwa na hamu ya kufanya kazi hata saa za ziada.

"Inawezekana wakati mwingine mtumishi wa chini anafanya kazi hadi unamuonea huruma, anafanya vile kwasababu ana nguvu ya kutosha anahamasa moyoni ya kufanya kazi, mwingine anaweza kufanya kazi kwa kuogopa na kulazimishwa,"alisema.

Waziri huyo alisema si vyema kiongozi kushindwa kutengeneza hamasa kwa watu walio chini yake kwa kuwa watakuwa na watumishi wanaowaongoza wenye hasira na serikali yao.

"Licha ya kufanya investment (uwekezaji) kubwa ya miradi yetu huku wananchi inawezekana wapo 'happy' (wanafuraha), lakini safu hii ambayo tunawaelekeza wawahudumie wananchi wanawezekana wakawa hawana hamasa ya utendaji kazi,"alisema.

Aliwataka kubadilisha utendaji wao wa kazi na kukuza hamasa kwa watumishi.

"Naamini tukifanya hivi tutakuwa na jeshi kubwa lenye hamasa ya watu, wale wanaofanya mambo ya ovyo tusiwafumbie macho,"alisema.

# PM kufungua kongamano la uwezeshaji

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI Mkuu Kassim, Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kongamano la nne la taifa la uwezeshaji wananchi kiuchumi ambalo linatarajia kufanyika Juni 15, mwaka huu.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi (NEEC), Bengi Issa, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema kongamano hilo litawakutanisha pamoja wadau wote kutoka wizara, idara, taasisi za umma na sekta binafsi.

"Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa atakuwa mgeni rasmi katika kongamano hili na atazindua ripoti ya mwaka ya uwezeshaji wananchi na kuwatambua wadau wa uwezeshaji waliofanya vizuri kutoka kwenye wizara, idara, taasisi za umma na sekta binafsi kwa kuwapa tuzo na vikombe na vyeti," alisema Issa.

Alisema kongamano hilo lenye kaulimbiu inayosema, 'Wezesha Watanzania kujenga Viwanda' lina lengo la kujadili kwa pamoja wadau namna ya kufikia ndoto ya kuwa na uchumi wa viwanda.

"Kama kaulimbiu inavyojieleza, tumeweka ujumbe huo kwa sababu tunaamini kuwezesha wananchi kujenga viwanda vitakavyotoa ajira nyingi, vitakavyowezesha wakulima kuzalisha mazao mengi na kuacha kuuza malighafi nje ya nchi," alisema.

Alieleza zaidi kuwa, katika kongamano hilo pia mada mbalimbali zitaibuliwa na waendesha mijadala ili kushirikishana uzoefu katika masuala ya uwezeshaji wananchi na hasa katika eneo la viwanda.

Aidha, aliwataka wadau wa uwezeshaji kuhudhuria kongamano hilo lenye lengo la kuhamasisha ushiriki wa wananchi, sekta za umma na binafsi kukuza uchumi wa nchi kupitia sekta ya viwanda.



Kikosi kazi cha dharura cha shirika la umeme la TANESCO, wilaya ya Temeke, wakikarabati nguzo iliyodondoka kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, katika Barabara ya Mwanga, eneo la Yombo Machimbo, jijini Dar es Salaam juzi, ambapo wananchi wa eneo hilo waliwapongeza kwa kufika haraka eneo la tukio na kuepusha hatari ambayo ingeweza kujitokeza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kisena, mkewe waunganishwa kesi moja

**Na Hellen Mwango**

WANAFAMILIA wawili akiwamo Mkurugenzi wa Kampuni ya Mabasi Yaendayo haraka Dar es Salaam (Udart), Robert Kisena (46), mke wake Frorencia Mshauri maarufu kama Frolence Membe (43) na wenzao watatu, wameunganishwa katika kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kutakatisha fedha na kusababisha hasara ya Sh. bilioni 2.4 kwa kampuni hiyo.

Jana saa 3:45 asubuhi, washtakiwa hao walipandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustine Rwizile na kufutiwa mashtaka chini ya Kifungu cha 91 kidogo cha (1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA).

Washtakiwa walifikishwa mahakamani kwa tarehe tofauti wakikabiliwa na mashtaka 19 katika kesi zao mbili tofauti.

Hata hivyo, upande wa Jamhuri uliomba kuwaondolea watuhumiwa hao mashtaka chini ya kifungu hicho cha sheria lakini baadaye walikamatwa ma kuunganishwa kisha kusomewa hati moja yenye mashtaka 19. Pia waliunganishwa na kufanya idadi yao kufikia watano.

Wakili wa Serikali, Glory Mwenda, alidai kuwa upande wa Jamhuri unaomba mahakama kuwafutia mashtaka chini ya kifungu cha 91 (1) cha Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) sura 20 iliyofanyiwa marejeo 2002 kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) hana nia ya kuendelea na kesi hizo. Mahakama iliridhia

INAENDELEA UK.8

# MNH yataka ufumbuzi kwenye utafiti

**Na Mary Geofrey**

MKURUGENZI wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Prof. Laurance Museru, amesema ili kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazoikabili sekta ya afya nchini, kuna haja ya kuendelea kufanya utafiti mwingi unaowekwa katika lugha rahisi.

Prof. Museru aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua kongamano la kwanza la kisayansi lenye kaulimbiu inayosema, 'Kutafsiri tafiti kwenda kwenye utendaji'.

"Hatuwezi kutoa tiba kama watu wengine hawajui wanachokifanya utafiti wa kitabibu unasaidia kuongeza ubora wa huduma wanazozitoa ingawa kwa bahati mbaya hatutoi kipaumbele, utakuta kuna makongamano kama haya, lakini wahudhuriaji ni wachache," alisema Prof. Museru.

Alisema utafiti huo pia ukiwekwa katika lugha rahisi utawezesha watoa huduma ya afya nao kufahamu kilichoandikwa na kusaidia kuboresha sekta hiyo.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Muhimbili, Prof. Charles Majinge, alisema amekuwa akipatiwa taarifa kuhusu hatua mbalimbali ambazo uongozi umekuwa ukichukua katika kuhamasisha ufanyaji wa utafiti katika maeneo ya kutoa huduma ikiwa ni pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya utafiti na makongamano.

Alisema katika kuwaunga mkono alitoa ahadi ya zawadi kwa ajili ya wale watakaojitokeza kufanya vizuri katika nyanja mbalimbali za tafiti.

Alisema utafiti mwingi umeonyesha kuwa kutengeneza miongozo na vipaumbele kwenye sekta ya afya kunasaidia kuokoa fedha nyingi.

Alisema jambo la msingi katika kufanya utafiti huo ni kuhakikisha usifanye kutegemea utajiri.

Naye Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita, alisema utafiti utakuwa na tija kama utatumika na kama hautumiki ni uharibifu wa fedha umma.

# DC Jokate awaasa vijana kutumia mitandao kwa manufaa

**Na Zuwena Shame**

VIJANA nchini wametakiwa kutumia mitandao ya kijamii kujiletelea mafanikio kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, alitoa ushauri huo wakati wa mdahalo wa kujadili changamoto mbalimbali zinazomkabili mtoto wa kike na mwanamke katika Siku ya Familia iliyoandaliwa na Shirika la Plan International nchini.

Mwegelo alisema vijana wengi kwa sasa wanatumia mitandao ya kijamii, lakini hawaitumii kwa usahihi kujiletea maendeleo ya kiuchumi na elimu badala yake wanaitumia kusambaza habari za uongo na umbea.

Alisema vijana wakishikamana na kutumia mitandao vizuri kwa kujadili masuala ya msingi kama elimu na jinsi ya kujikwamua kiuchumi, wanaweza kufika mbali na kupiga hatua kimaendeleo.


"Hii mitandao ya kijamii ni kama kisu, unaweza kukitumia vizuri na ukanufaika na unaweza kutumia vibaya ukapata athari mbalimbali. Hivyo tujue kuwa ni nyenzo muhimu kama ikitumiwa vizuri kwenye kuleta au kutafuta maendeleo," alisema Jokate.

Alisema mitandao ya kijamii imeonyesha mafanikio makubwa katika kampeni ya 'Tokomeza Ziro' wilayani mwake kwa kuwa amepiga hatua katika kutokomeza ziro mashuleni wilayani Kisarawe.

"Kampeni yetu ya Tokomeza Ziro Kisarawe imepata manufaa kwa kuwa watu wengi wametumia mitandao ya kijamii kutusaidia kwa hali na mali," alisema Jokate na kuwataka wasichana nchini kusoma kwa bidii na kuepuka vishawishi ili waweze kufikia ndoto zao za kielimu na kimaisha pia.

Mkurugenzi wa Plan International nchini, Gwyneth Wong, aliiomba serikali na wadau mbalimbali kuweka nguvu na jitihata zaidi

INAENDELEA UK.8

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Hatua ya kuwafuatilia tembo ina lengo zuri*

**TAARIFA** kwamba zaidi ya Sh. milioni 800 zinatarajiwa kutumika kwenye zoezi la kuwafungia tembo mkanda wenye mawasiliano na satelaiti, unaotumika kurusha taarifa ya mahali mnyama alipo, ni nzuri na zinahitaji kuungwa mkono.

Zoezi hilo lilizinduliwa mapema wiki hii katika Hifadhi ya Jamii ya Makao wilayani Meatu Mkoa wa Simiyu, na Waziri wa Maliasili na Utalii, Kamis Kigwangalla.

Waziri Kigwangalla alisema idadi ya tembo imeongezeka kutokana na kupungua kwa ujangili, na kuongeza kuwa teknolojia hiyo itasaidia kujua tembo aliko au anakoelekea.

Alisema zoezi hilo litasaidia pia kuwalinda tembo sambamba na mali za wananchi, huku ikitambua idadi halisi ya tembo wanaoongezeka.

Alisema kuwa makundi ya tembo yameongezeka, ukijaribu kupita kwenye hifadhi mbalimbali na mapori ya akiba idadi ya tembo na wadogo ni kubwa.

Itakumbukwa kuwa miaka kadhaa iliyopita tembo katika hifadhi na mapori yetu ya akiba walipungua kutokana na kushamiri kwa vitendo vya ujangili, jambo ambalo liliiathiri sekta ya utalii na kuikosesha nchi mapato.

Tunakumbuka pia jinsi serikali ya awamu ya nne ilivyoanza kuchukua hatua, kwa kuanzisha operesheni kadhaa za kulinda hifadhi zetu dhidi ya vitendo vya majangili katika maeneo yote ya nchi. Mojawapo ya oparesheni hizo ni ya Tokomeza, ambayo licha ya kuwakamata watuhumiwa wengi wa vitendo vya ujangili, ililalamikiwa na baadhi ya wananchi kwa madai kuwa watekelezaji wake walikiuka haki za binadamu.

Hata, hivyo kwa namna moja au nyingine, operesheni hiyo isingeweza kuepukika kutokana na hali ilipokuwa imefikia. Tunasema hivyo kwa kuwa ilianza kuonekana kuwa rasilimali za taifa zinawanufausha watu wachache (majangili na mawakala wao) badala ya serikali na wananchi).

Kadhalika, zilishaanza kuonekana dalili za kuitia dosari nchi yetu kwamba haichukui hati madhubuti za kulinda rasilimali zetu hususan wanyamapori, hivyo kuwa kitovu cha usafirishaji wa meno ya tembo kwenda nje.

Vita dhidi ya ujangili iliyoendelezwa na serikali ya awamu ya tano, imesaidia sana kuongeza idadi ya tembo na kuirejeshea heshima nchi yetu.

Pamoja na hayo, tunaelewa changamoto kubwa iliyoko sasa, ya wanyama wakali hususan tembo kuondoka mara kwa mara katika hifadhi na mapori ya akiba na kuingia kwenye makazi ya wananchi kisha kusababisha uharibifu wa mashamba na hata kuwadhuru binadamu.

Matukio mengi ya aina hiyo yamekuwa yakiripotiwa, hivyo ni hatua ya kutia moyo kusikia kwamba zimetengwa fedha hizo kwa ajili ya kufuatilia tembo popote walipo.

Tunaipongeza hatua hiyo tukiamini kuwa itasaidia kuwa na taarifa sahihi kuhusu wanyama hao, kwa kuwa itajulikana waliko na wanakoelekea pale watakapojaribu kuondoka kwenye hifadhi.


Vile vile, usalama wao utakuwa mkubwa kwa kuwa wamlaka husika zitakuwa na taarifa, hivyo itakuwa rahisi kudhibiti hata majaribio ya ujangili dhidi yao.

Kwa upande mwingine, wananchi ambao wanaishi karibu na hifadhi pamoja na mapori ya akiba wataondolewa usumbufu wa kuharibuwa mali zao na tishio la usalama wa maisha yao, kwa kuwa itakuwa rahisi mamlaka husika kuwadhibiti haraka kabla ya kuleta madhara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

## *Mvua hizi zitufunze jambo*

Na Yasmine Protace

**SOTE** tunakubaliana kuwa mvua ni baraka kwetu sote na kila inaponyesha, wapo wengi wanaofurahi kutokana kupata maji, ambayo yana matumizi mengi kupita kiasi; nyumbani, shambani na sehemu za uzalishaji kama vile viwandani.

Mvua hiyo inaponyesha, baadhi ya watu wanaifafanua kiimani zaidi, zaidi ya mtazamo wa kiikolojia iliyozoeleka, wakitamka: "Ni Baraka Kutoka kwa Mwenyezi Mungu."

Ni ufafanuzi unaoenda mbali katika lugha ya ushuhuda kwamba, kila mvua zinapogoma au kuchelewa kunyesha, viongozi wa dini hushirikishwa kupitia nguvu ya maombi yao, ili mvua zinyeshe na kufakikisha kupunguza joto, upatikanaji maji na mazao yanusurike.

Mvua zinapopatikana, mara moja neema zinazoambatana nazo hushuhudiwa. Lakini, katika upande wa pili wa shilingi ambao kidole changu kinaelekeza, kuna tabia zisizofaa kutokana na mvua hizo.

Hapo ninajielekeza mijini, tena nikisonga kule kunakojulikana 'Uswahilini.' Hapo ndipo kunapotokea ushuhuda wa yasiyo ya kistaarabu, kwa maana ya maji machafu kutoka katika yaliyo na vinyesi.

Pia tumeona, mvua hizi ziliponyesha katika baadhi ya mikoa. Zimeleta changamoto kuanzia uharibifu wa miundombinu ya umma, makazi na adha kubwa kwa jamii.

Nikiamua kuwa mahsusi kwa jiji la Dar es Salaam, nako kuna adha yake kubwa. Mvua imeleta changamoto kubwa kwa wakazi wake.

Sote tulioko jijini tumeona namna baadhi ya miundombinu ya barabara imekuwa haipitiki na kukatika kwa mawasiliano kuingia upande mwingine.

Katika barabara ya Morogoro ambayo ni kubwa na muhimu ndani ya jiji, tumeona mawasiliano ya kuingia mjini, yaani katika maeneo kama Posta, Mnazi Mmoja na Kariakoo.

Hali haikuwa nafuu hata kidogo, magari kutoka nje ya mji, yalikuwa yanaishia Magomeni Mapipa na hapo abiria kia mmoja kwa mikakati yake binafsi, alilazimka kujipanga namna atavyofika aendako huko mjini.

Ndipo inakuja simulizi ya baadhi ya watu kulazimika kupada usafiri wa baiskeli za magurudumu matatu, maarufu Gutta wavushwe kwa kwenye maji mengi kwa tozo la nauli kati ya Sh. 500 hadi 1000, wakielekea kama Posta, Kariakoo na kwingineko, baadhi wakiwa na safari ya mbali zaidi kufikia maeneo kama Kigamboni.

Hapo mabasi ya huduma za Mwendokasi, yanayotegemewa sana na wakazi wa Barabara ya Morogoro kati ya Mbezi na Mjini na Barabara ya Bibi Titi, kati ya eneo la Kinondoni Morocco na Magomeni, huduma hiyo kwao ilisitishwa.

Sababu iko wazi, miundombinu na hasa iliko daraja la Jangwani, kulifurika maji na athari zisambaaa, zikiwamo shule kufunga kwa muda.

Kuna shule nazo ziliguswa moja kwa moja, baadhi ya madarasa yalijaa maji, walimu na wanafunzi wakashindwa kuhudhuria vipindi, kwa mujibu wa taratibu na ratiba zao.

Kimsingi, mvua hizo zinaponyesha tumeona hata baadhi ya watu wanazibua majitaka, pasipo kujali afya za watoto wanaocheza, wapita njia, wakazi jirani na wengine ambao kwa njia moja au nyingine ni wahusika.

Katika kipindi hicho cha mvua, tumeona magari madogo yanazimika, pindi yanapopita katika madimbwi ya maji hayo, hapo inazuka kero ya foleni barabarani.

Sasa, kutoka na mvua hizi ambazo hazijaisha, jamii tunatakiwa kujifunza kitu.Wahusika wasimamizi wa miundombinu husika, wanapaswa kuzitumia changamoto hizo kwa kuboresha miundombinu, ili kuwapunguzia kero kutoka kwa wananchi.

Kwa sasa, barabara za mitaani hazipitiki. Mashimo yamekuwa mengi, pia baadhi ya masoko kwa sasa yamejaa tope na hata watu kuingia sokoni, unatakiwa kuvaa mabuti kutokana na kuwapo na tope jingi na uchafu wa kila namna.

HABARI KITAIFA

## Waamini makanisa kikatoliki wapewa elimu ya bima

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya Wakala wa Bima ya Acclavia, imeanzisha programu ya kutoa elimu ya utumiaji wa bima kwa waamini wa makanisa ya kikatoliki kwa lengo la kuhakikisha wanakuwa na uhakika wa matibabu, huduma za majanga na msiba.

Akizungumza jijini Dar es Salaam ikiwa ni mwendelezo wa utoaji wa mafunzo kwa waumini wa Kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mratibu wa Mafunzo wa Kampuni ya Wakala wa Bima ya Acclavia, Rosemary Kiambo, alisema lengo kuu ni kuhakikisha wanalinda afya za waumini pamoja na kuhakikisha wanapata huduma nyingine kupitia bima ya afya.

"Katika programu hii, tunahudumia matibabu ya afya, tunatoa huduma ya maisha ambayo imejikita katika majanga ya msiba ambako tumeona kwamba isaidie kuondoa changamoto za michango ya mara kwa mara ambayo tumekuwa tukiipata hadi kufikia kuchangishana pale tunapofiwa," alisema Kiambo na kuongeza:

"Bima hii yenyewe itakuwa inasaidia gharama za msiba, badala ya kuchangishana hiyo ndiyo inatumika na kuondoa changamoto kwa wanaobaki hai."

Alisema kwa sasa wameanza kwenye makanisa ya Katoliki yaliyopo katika jiji la Dar es Salaam na baada ya hapo watafika makanisa mengine na kwa Watanzania wote.

"Hii ni programu maalum ambayo ililenga Wakatoliki walioko jijini Dar es Salaam na mpaka sasa tumeshatembelea zaidi ya parokia 50, lakini tunatarajia tukishamaliza hapa tutakwenda na mikoa mbalimbali na kwa Watanzania wote," alisema Kiambo.

Alisema wameamua kufanya hivyo kwa sababu Watanzania wengi walikuwa hawana uelewa wa bima, wakiona ni ya kundi fulani, hivyo programu hiyo ni kwa ajili ya kuwaongezea uelewa na kuwasaidia kufahamu umuhimu wake.

"Pamoja na kwamba bima imekuwa inatumika kwa kipindi kirefu kwa ajili ya masuala ya afya, lakini Watanzania walio wengi bado hawajaona umuhimu na hawajiungi, kwa hiyo wanapopata matatizo wanakosa msaada au kuanza kuchangishana, lakini programu hii ya bima ambayo tumeianzisha itasaidia kuhudumia mtu anapofiwa, anapougua na huduma nyingine," alisema Kiambo.

Alisema wanatarajia ifikapo 2020 kila Mkatoliki awe amepata bima ya afya. Mshiriki wa semina hiyo, Maiko Gama, alisema elimu hiyo imewasaidia kuwafungua akili na wanaamini changamoto ambazo walikuwa wanazipata za kushindwa kujigharamia katika vipindi vigumu vya matatizo ya kiafya na vifo zitaisha.

"Unajua zamani tulikuwa tunachukulia huduma hizi za bima kama kamari, tunashukuru sana kampuni ya Acclavia imetufungua akili na tunaona itakuwa msaada mkubwa kwetu," alisema Gama.

# ACT-Wazalendo watoa msimamo uchaguzi serikali za mitaa

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimetoa pendekezo la kuundwa chombo kitakachokuwa kinaratibu upatikanaji wa watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), ambacho kitakuwa na misingi ya uadilifu, shirikishi na cha uwazi.

Pia kimependekeza wajumbe wa chombo hicho wawe na hadhi ya ujaji na mwenyekiti wake awe ni Jaji wa Mahakama Kuu, kishirikishe wadau kutoka vyama vya siasa hususani upinzani, asasi za kiraia na utumishi wa umma. Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mawasiliano ya Umma wa chama hicho, Ado Shaibu, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akipongeza uamuzi uliotolewa na Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kuhusu wakurugenzi wa wilaya, Jiji na Manispaa kutosimamia chaguzi zozote nchini. Mei 10, mwaka huu Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, ilibatilisha kifungu cha sheria cha 7(3) kinachowaruhusu Wakurugenzi wa Manispaa na Halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi nchini.

"Sisi ACT-Wazalendo tunapongeza uamuzi uliotolewa na Mahakama Kuu, tunawapongeza majaji wote waliotoa hukumu hiyo, uamuzi uliofanyika ni mkumbwa na utakuwa wa kihistoria nchini, tunampongeza wakili Fatma Karume na Bob Chacha Wangwe kwa uamuzi wao wa kusimamia kesi hiyo," alisema Shaibu na kuongeza:

"Watanzania watawakumbuka kwa uamuzi wao wa kihistoria ambao umeacha alama ya kudumu katika nchi yetu. Tangu mfumo wa vyama vingi ulipoanza nchini mwaka 1992, Tume tatu za Jaji Warioba, Jaji kisanga, Jaji Nyarari zote zilikuwa za wananchi na zilikuwa zikizungumzia masuala ya mabadiliko katika Nec".

Alisema tume zote tatu zilizungumza kwa uwazi kuhusu maoni ya wananchi kutaka mageuzi katika Nec. Shaibu alisema Tume ya Jaji Nyalali ilipendekeza kufumuliwa kwa Nec, hivyo hivyo Tume ya Jaji Kisanga na Jaji Warioba zote zilipendekeza kufanyika kwa marekebisho katika Nec.

Alisema Watanzania wengi wamekuwa hawaridhishwi na uendeshaji wa Nec na ndiyo sababu kila tume ilikuwa inakuja na maoni yaliyokuwa yanafanana. Alisema Mahakama Kuu imeonyesha mfano uliotukuka katika kutoa uamuzi huo na kwamba ni wakati sasa wa Nec kujiandaa kibajeti kwa kuwatafuta wasimamizi wa uchaguzi katika ngazi za wilaya, manispaa na majiji.

"Tunataka chombo ambacho tukikitazama tunasema hiki ni chombo chetu cha kusimamia uchaguzi, Tunataka Nec ndiyo wawe wasimamizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa na siyo Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Aisema ni vyema Nec ikaanza sasa kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.



Wachuuzi wa vikapu wakisaka wateja katika eneo la Msimbazi centre, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwanafunzi shule ya awali afariki dunia katika ajali

**Na Mary Geofrey**

MWANAFUNZI wa awali katika Shule ya Silva Lifu, Osligi Emanuel (3) amefariki dunia papo hapo kufuatia ajali iliyotokea eneo la Himiti, wilayani Babati, mkoani Manyara.

Ajali hiyo ilitokea jana saa 12:20 asubuhi baada ya basi la abiria la Mtei Express linalofanya safari zake kati ya Babati-Dodoma, lenye namba za usajili T 299 AXP kugongana uso kwa uso na gari ya wanafunzi aina ya Nisani lenye namba za usajili T 390 BHZ. Katika ajali hiyo watu wanne walijeruhiwa akiwamo mwanafunzi Lyatiness David (6), mwalimu Francis Mollel (39), dereva wa gari la wanafunzi Daniel Godfrey (25) na kondakta wa basi la Mtei, Paul Shilala (24).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Augustino Senga, alilieleza Nipashe kwa njia ya simu kuwa, dereva wa basi hilo alisababisha ajali hiyo wakati akijaribu kulipita gari lingine na kwenda kugongana uso kwa uso na gari hilo ya wanafunzi.

"Ajali hiyo ilitokea leo (jana) asubuhi wakati dereva wa basi la abiria akijaribu kulipita gari lililokuwa mbele yake na kuligonga gari la wanafunzi na kusababisha kifo cha mwanafunzi mmoja, mtoto mwenye miaka mitatu na kujeruhi watu wengine wanne," alisema.

Kamanda Senga alisema majeruhi wote walikimbizwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mrara kwa ajili ya kupata matibabu na kueleza kuwa waliumia zaidi maeneo ya miguuni, mikononi na michubuko sehemu za kichwani.

Alitoa tahadhari kwa madereva wote kuwa waangalifu wakati wa msimu wa mvua za masika kwa sababu barabara zinateleza na hasa mkoa huo ambao ukungu unatanda wakati wa asubuhi.

Alieleza kuwa, Jeshi hilo linaendelea kumsaka dereva aliyehusika na ajali hiyo, Japhet Lyimo ili kuchukuliwa hatua za kisheria.

# Shahidi adai alipigwa jiwe na kupoteza fahamu

INATOKA UK. 4

Vicent Mashinji, Mbunge wa Iringa mjini, Peter Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Mbunge wa Kawe, Mdee na John Heche.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari mosi na Februari 16, mwaka jana na wenzake wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Ilidaiwa kuwa Februari 16, mwaka huu Bulaya alishawishi kutenda kosa la jinai katika viwanja vya Buibui vilivyopo Kinondoni,jijini Dar es Salaam alishawishi wakazi wa eneo hilo kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu.

Ilidaiwa Februari 16,mwaka huu barabara ya Kawawa eneo la Mkwajuni wilaya ya Kinondoni kwa pamoja washtakiwa na wenzao zaidi ya 12, walifanya mkusanyiko na kukaidi amri halali ya ofisa wa jeshi la polisi Gerald Ngiichi na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi kujeruhiwa.

Ilidaiwa siku ya tukio la kwanza na la pili, katika viwanja vya Buibui vilivyopo Kinondoni jijini Dar es Salaam, kwenye mkutano wa hadhara mshitakiwa Heche alitoa lugha ya kuchochea chuki alitamka matamshi kwamba "Kesho patachimbika upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii...wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano...watu wanapotea...watu wanauawa, wanaokotwa kwenye mitaro lazima ukome... "alinukuliwa na kudaiwa kuwa maneno yaliyoelekea kuleta chuki kati ya serikali na Watanzania.

Washtakiwa wote waliposomewa mashtaka yao kwa nyakati tofauti walikana.

## DC Jokate awaasa vijana kutumia mitandao kwa manufaa

INATOKA UK. 5

katika kutatua changamoto mbalimbali zinazomkabili mtoto wa kike ikiwamo ukatili wa kijinsia kama mimba za utotoni na ukeketaji.

Wong alisema kuwa mdahalo huo pia ulijumuisha vijana hasa wa kike ili kujadili changamoto zao na jinsi ya kuzitatua kwa kutoa elimu kwa jamii zinazowazunguka.

Dk. Katanta Simwanze kutoka idara ya afya, jinsia na makundi maalumu kutoka Plan international, alisema wamewawezesha vijana kwa kupewa elimu ya masuala ya athari za mimba za utotoni, ukeketeaji na afya kwa wasichana ili kuongea na vijana wenzao katika ngazi za jamii.

Naye mwenyetiti wa vijana kutoka Youth for change inayofadhiliwa na Lian international, Neema Olle Ndemno, alisema kuwa kumekuwa na mkingamano wa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ambayo inamruhusu mtoto wa kike kuolewa chini ya umri wa miaka 18.



Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Reli nchini (TRAWU), Lomitu Ole Saitabau, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akikanusha taarifa kuwa chama hicho, kimemuongopea Rais. Kushoto ni Katibu Mkuu chama hicho, Nashon Malyeri. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kisena, mkewe waunganishwa kesi moja

INATOKA UK. 5

na kuwaachia huru.

Pia wahtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka manne ya utakatishaji wa fedha, mashtaka manne ya kutoa nyaraka za uongo, manne ya kughushi, mawili kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kusababisha hasara.

Mbali na Kisena, washtakiwa wengine wanaokabiliwa na kesi hiyo ni Kulwa Kisena (33), Charles Newe (47) na Chen Shi (32).

Ilidaiwa kuwa kati ya oktoba 2012 mpaka Mei 31, 2018 washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari Mosi, 2011 na Mei 31, 2018 katika mahali tofauti wakiwa na watu wengine, waliratibu shughuli za kihalifu huku wakijua kufanya hivyo ni kosa la kisheria.

Katika shtaka la pili, kati ya Januari Mosi, 2015 na Desemba 31, 2017 katika eneo la Jangwani, washtakiwa wakiwa wakurugenzi wa Kampuni ya Zenon Oil Gas Limited walijenga kituo cha mafuta kinachoitwa. Zenon Oil and Gas katika karakana ya Kampuni ya Udart bila kuwa na kibali kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma na Nishati na Maji (Ewura).

Shtaka la tatu, kati ya Januari Mosi, 2015 na Desemba 31,2017 katika eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam, washtakiwa wakiwa wakurugenzi wa kampuni hiyo kwa pamoja walianzisha biashara ya kuuza mafuta ya petroli katika eneo ambalo halijaruhusiwa. Katika shtaka la nne la utakatishaji, kati ya Mei 25, 2015 na Desemba 31, 2015 wakiwa jijini Dar es Salaam, washtakiwa waliibia Sh1, 216,145, 374 mali ya Kampuni ya Udart.

Shtaka la tano la utakatishaji wa fedha, inadaiwa kati ya Mei 25, 2015 na Desemba 31, 2016 katika jiji la Dar es Salaam, Robert Kulwa Charles na Frolencia wakiwa na lengo la kuficha uhalisia walibadilisha thamani ya ani ya Sh. 1, 216, 145, 374 kwa kuyauza wakati akijua mafuta hayo ni zao la uhalifu.

Mwenda alidai shtaka la sita ni utakatishaji wa fedha washtakiwa hao wanadaiwa kuwa ambapo kati ya Mei 25, 2015 na Desemba 31, 2016 wakiwa jijini Dar es Salaam walimiliki Sh. 1,216,145,374 huku wakijua ni zao la kosa la wizi.

Katika shtaka la saba ilidaiwa kati ya Mei 25, 2015 na Desemba 31, 2016 akiwa jijini Dar es Salaam kwa makusudi aliisababishia hasara UDART ya Sh.2.414, 326, 260.70 Ilidaiwa kuwa Membe na Kisena wanakabiliwa na shtaka lakujenga kituo cha mafuta bila kibali cha Ewura.

Hakimu alisema washtakiwa hawatakiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi bila kibali cha DPP au upelelezi utakapokamilika itahamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa.

Jamhuri ulidai kuwa upelelezi bado haujakamilika na uliomba tarehe ya kutajwa.

Hakimu Rwizile alisema washtakiwa hawatakiwi kujibu chochote kwa kuwa mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Alisema kesi hiyo itatajwa Mei 28, mwaka huu na washtakiwa wapelekwe mahabusu.

# Biashara 16,000 zafungwa miezi 10

INATOKA UK. 2

kutambulika kwa mujibu wa sheria.

"Mambo mengi yanayofanyika, ni kutokana na sheria zilizotungwa hapa bungeni. Kwa mfano, Sheria ya Korosho Namba 12 inasema ukikutwa na korosho kama huna kibali cha Bodi ya Korosho, unapaswa kukamatwa. Tukiamua kufanya kama sheria inavyotaka, hata hao wakulima tutawakamata," alisema.

Mgumba alisema serikali iko kwenye mchakato wa kupitia sheria na Sera ya Kilimo ya Mwaka 2003 ili kuja na sheria na sera yenye kuendana na mazingira yaliyopo.

Alisema kuna wakulima wa korosho wanaoidai serikali zaidi ya Sh. bilioni 102 kati Sh. bilioni 700, baada ya kuwa imewalipa wakulima zaidi ya Sh. bilioni 600.

Mgumba pia alisema kulinda viwanda vya ndani ni jambo la msingi, lakini si vyote vinafungwa kwa madai ya mipango mibovu ya serikali.

"Kwa mfano, viwanda viwili vya alizeti mkoani Singida vimefungwa kutokana na ukosefu wa malighafi nchini, sasa ni muhimu pia tukahamasisha wakulima katika uzalishaji wa malighafi za kutosha kuviwezesha viwanda," alisema.

Mgumba pia asema serikali iko katika mchakato wa kuingia mkataba maalum na wanunuzi wa mbaazi baada ya kubaini kulifanya makosa ya kutoingia mkataba na wanunuzi wa awali wa zao hilo.

**UTITIRI WA MAMLAKA**

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, alisema serikali imeanza kuitafutia ufumbuzi changamoto iliyolalamikiwa na wabunge wengi ya utitiri wa taasisi za udhibiti.

"Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Viwanda, imeanza kuchukua hatua. Tayari Waziri Mkuu alikwishachukua hatua kwa kuitisha kikao na kingine amekiitisha Jumamosi ambapo kitapitia changamoto na vikwazo vinavyochangia biashara kutokukua," alisema.

Waziri Kairuki alisema zipo tozo ambazo zimependekezwa kuondolewa na kupunguzwa kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha pindi utakapowasilishwa.

Alisema wizara pia imeanza mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Uwekezaji kwa kuwa serikali inatambua sheria hiyo ni ya muda mrefu tangu mwaka 1997 na haiendani na mazingira ya sasa.

# Mkataba uwekezaji waibua mvutano kanisa, mbunge

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya viongozi wa Kanisa la Evangelistic Asemblies of God Tanzania (EAGT), wameibuka na kutilia shaka mikataba iliyoingia kanisa hilo ukiwemo wa miaka 47 ijayo unaomhusu mwekezaji wa ndani.

Mwekezaji huyo ametajwa kwa jina la Jumanne Kishimba ambaye pia ni Mbunge wa Kahama Mjini mkoani Shinyanga na mmiliki wa Imalaseko Investment Ltd.

Kishimba anadaiwa kuingia mkataba mwaka 2010 wa kujenga jengo kwenye kiwanja kinachomilikiwa na kanisa hilo kilichopo pembezoni mwa Barabara ya Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Kanisa hilo limekumbwa na mgogoro huo tangu kufariki kwa aliyekuwa Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, Moses Kulola na aliyekuwa Katibu, Mchungaji Brown Mwakipesile, kuchaguliwa kuwa Askofu Mkuu.

Baadhi ya wachungaji wanamtuhumu Askofu Mwakipesile kuhusika na mikataba hiyo ambayo inadaiwa kuwa haina maslahi kwa kanisa kwa kuwa kuna baadhi ya mambo ambayo yanaashiria udanganyifu.

Mchungaji Benson Kitotonka wa jijini Mwanza, aliliambia gazeti hili jana kuwa, anakumbuka makanisa yalichangishwa kwaajili ya ujenzi wa jengo hilo hivyo wanashangaa kusikia kuwa mwekezaji ndiye aliyejenga.

"Nakumbuka aliyekuwa Askofu Mkuu, mzee Kulola, alituhamasisha kuchangia ujenzi wa majengo hayo, nakumbuka kule kwetu walikuja baadhi ya viongozi wakiwa wameongozwa na Makamu wa Askofu John Mahene, walisimamia michango wenyewe," alisema.

Alisema kuwa kiini cha mgogoro katika kanisa hilo ni baada ya watu kuanza kuhoji kuhusu mapato na matumizi.

"Bahati mbaya kwenye kanisa letu mapato na matumizi huwa hayasomwi, ukitaka kuzungumza kuhoji kwenye mkutano wowote mkuu unaambiwa kaa chini," alisema Mchungaji Kitotonka.

Kwa upande wake, Mchungaji Yared Lesilwa wa kanisa la EAGT Aman Kikuyu East jijini Dodoma, alisema majengo hayo hayajalisaidia kanisa kwa chochote kwa kuwa hakuna taarifa za mapato na matumizi walizosomewa hadi sasa.

**MAJIBU YA KISHIMBA**

Mwekezaji Kishimba alipohojiwa kuhusu madai hayo alisema waliandikiana mkataba wa halali na viongozi wa kanisa hilo na

INAENDELEA UK. 24



Wananchi wakiangalia gari aina ya Hiace yenye namba za usajili T 736 DJF, baada ya kupinduka katika kijiji cha Kisuke lilipokuwa linatoka Ulowa kwenda Kahama Mjini mkoani Shinyanga. Abiria 30 walijeruhiwa, huku chanzo kikielezwa ni kupasuka tairi ya nyuma.
**PICHA: MARCO MADUHU**

# Serikali yaweka mikakati ufugaji wa samaki

**Na Mary Geofrey**

KUTOKANA na uhaba wa samaki nchini, Serikali imeweka mikakati ya kuongeza kasi ya ufugaji wa viumbe hao kwa ajili ya kutosheleza soko la ndani na nje.

Kwa wastani mtu mmoja anatakiwa kula samaki kilogramu 20 Kwa mwaka, lakini nchini mtu mmoja anakula kilogramu 7.6 Kwa mwaka.

Hayo yalielezwa jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Utunzaji Viumbe Maji wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Nazael Madala, wakati akizungumza katika mkutano uliowakutanisha wadau wa viumbe hai wakiwamo watafiti, wafugaji na wanafunzi kwa lengo la kijadili namna ya kuboresha sekta viumbe hao.

"Nchini tani 18,000 za samaki zinazalishwa kwa mwaka ambazo hazitoshelezi kulingana na mahitaji... Ili kukabiliana na uhaba huu sasa, tunahimiza wavuvi na wadau wengine kujikita kwenye ufugaji wa samaki," alisema Dk. Madala.

Alitaja sababu ya kuadimika samaki ni uvuvi haramu, uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Dk. Madala alisema hata hivyo katika kipindi cha miaka miwili kumekuwapo na kampeni za kuzuia uvuvi haramu zilizosaidia kupungua kwa uharibifu huo nchini.

Alisema matumizi ya mabomu na makokoro yamepungua, na kwamba wameendelea kutoa elimu ya uvuvi kwa jamii ili kumaliza kabisa changamoto hiyo.

Katibu wa Chama Cha Wakuzaji wa Viumbe Maji Tanzania (AAT), Geoffrey Rucho, alisema lengo la mkutano huo kuhakikisha utafiti uliofanywa kuhusu hali halisi ya viumbe hai nchini na kuwakutanisha wadau kuijadili na kuleta mabadiliko chanya katika sekta hiyo.

Naye Mtaalamu wa viumbe hai, Prof. Philip Bwathondi, alisema viumbe wa majini kama samaki wamepungua kwa sababu watumiaji wameongezeka na vifaa vya kuvulia vimeongezeka.

Alisema njia ya kuongeza viumbe hao ni kuanza kufuga na kusaidia wavuvi wengine kujikita kwenye kufuga na kuongeza uzalishaji.

Alisema pia njia nyingine ni kufuga samaki wadogo ambao wakifika umri wa ukuaji wanamwagwa kwenye eneo moja la ukuaji ili kupunguza upungufu uliopo.

# Watoto 100 waugua saratani Muhimbili

**Na Mary Geofrey**

JUMLA ya watoto 100 wanaougua saratani mbalimbali ikiwamo ya macho, wamelazwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), wakiendelea kupatiwa matibabu. Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrance Museru, akiwaambia waandishi wa habari wakati akikabidhiwa msaada wa mashine za kutibu kansa ya macho kwa watoto zenye thamani ya Sh. milioni 170 zilizotolewa na Rotary Club ya Oysterbay jijini Dar es Salaam. Prof. Museru alisema takwimu hizo ni kwa mujibu idadi ya watoto waliokuwa wodini juzi na kwamba matibabu yao huchukua miezi mitatu hadi sita.

"Kwanza niwashukuru Rotary Club ya Oysterbay kwa msaada wao, msaada huu wa vifaa vya matibabu ni mkubwa utawezesha Muhimbili kufanya upasuaji kwa watoto wenye saratani za jicho ili mtoto aendelee kutumia jicho lililokuwa limepata madhara," alisema Prof. Museru.

Alisema Rotary Club wamekuwa wakitoa misaada hiyo katika kupunguza changamoto inayowakabili Muhimbi ya kutoa tiba sahihi kwa wagonjwa hao.

Aliahidi kuwa vifaa hivyo vitatumika kulingana na mahitaji, kuvitunza na kuendelea kutoa huduma kwa miaka mingi zaidi na vingine vitabaki Muhimbili na vingine watavipeleka tawi la Mloganzila. Alisema taasisi ya Kijamii ya Tumaini la Maisha imekuwa msaada mkubwa kwa watoto hao, ambao wamekuwa wakitoa dawa za kutibu na msaada wa malezi katika nyumba ya kuwalea wanapokuwa katika matibabu hospitalini hapo.

Naye Daktari Bingwa wa Macho kwa Watoto, Dk. Anna Sanyiwa, alisema vifaa walivyopatiwa ni vya muhimu na vinatibu uvimbe mapema kabla saratani haijasambaa.

Alisema kabla ya kuwapo kwa mashine hizo watoto walikuwa wanaondolewa macho, lakini kupitia mashine hizo macho hayataondolewa.

"Nitoe wito kwa wazazi kuwahisha watoto hospitali wanapoona watoto wao wanadalili za magonjwa ya macho kama vivimbe wa rangi nyeupe kwenye macho ili wawahi tiba hii," alisema Dk. Sanyiwa. Aidha, aliwataka wadau wengine wa maendeleo kuendelea kuchangia vifaa vya matibabu katika kusaidia kuokoa maisha ya watoto wanaougua saratani. Kaimu Mkurugenzi wa Rotary Club Oysterbay, Kirubakaran Ramakrishnan, alisema msaada huo ni muendelezo wa misaada ambayo wamekuwa wakitoa kwa watoto wenye saratani wa hospitali hiyo.



Naibu Waziri Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, akijibu swali bungeni, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MAELEZO**

# Serikali: Sheria ya SOSPA haijadhibiti ubakaji watoto

IMEELEZWA kuwa licha ya kufanyiwa marekebisho Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA) mwaka 2002 na kuongeza adhabu ili kukomesha vitendo vya ubakaji watoto nchini, lakini bado vimeendelea kuongezeka.

Kwa mujibu wa takwimu za hali ya uhalifu na matukio ya usalama barabarani, ubakaji umeongezeka kutoka matukio 394 Disemba 2015 hadi 2,984 Disemba 2017.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Najma Murtaza Giga.

Katika swali lake, Giga alisema Sheria hiyo ya mwaka 1998 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2002 ili kukomesha vitendo vya ubakaji wa watoto chini ya miaka 18 ambapo kwa atakayembaka mwanafunzi atakumbana na adhabu ya miaka 30 jela, huku atakayembaka mtoto chini ya miaka 10 atafungwa maisha.

"Je, tokea kupitishwa kwa sheria hii na marekebisho yake, ubakaji umepungua au kukoma hapa nchini, je, kama bado changamoto ipo serikali ina mpango mkakati gani mpya katika kupambana na kutokomeza ubakaji Tanzania?"alihoji.

Akijibu, Dk.Ndugulile alisema pamoja na adhabu hiyo ambayo ni kubwa ambayo ingefanya watu kuogopa kujihusisha na vitendo hivyo, bado ubakaji watoto nchini umeendelea kuongezeka.

"Ongezeko hili limetokana na jamii kutoa taarifa ya masuala ya ubakaji pindi yanapotokea," alisema.

Aidha, alisema serikali imetekeleza afua mbalimbali katika kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto, ikiwamo kuanzishwa kwa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto 10,988 katika ngazi za halmashauri, kata na vijiji kuanzisha vikundi vya malezi 1,184 na kuwezesha huduma ya simu kwa watoto.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Naibu Waziri huyo alisema serikali imeandaa Mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto 2017/18-2021/22 ambayo kupitia mpango huo serikali inatekeleza afua mbalimbali za kutoa elimu bure.

Pia, alisema kuandaa na kutoa elimu juu ya malezi chanya kupitia kitini cha malezi na makuzi na kuandaa mkakati wa mawasiliano wa kuelimisha wananchi kuachana na mila potofu.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alitaka kujua ni watu wangapi wamefikishwa kwenye vyombo vya sheria na wangapi wamepata adhabu hiyo.

"Vitendo hivi vinafanywa miongoni mwa ndugu zetu, kwanini serikali isitolewe ruhusa kwa jamii kuwatambua watu wanaofanya ubakaji ili waweze kujitenga na watu hao?"alihoji.

Akijibu, Dk. Ndugulile alisema matukio hayo mara nyingi yanafanywa na watu ambao wapo karibu na familia, lakini kesi zake hazifiki mwisho kutokana na familia kutotoa ushirikiano kwa vyombo vya dola.

"Wale watu waliohukumiwa na makosa ya ukatili wa kijinsia ukiwamo ubakaji kwenye nchi zingine huwa wanatambuliwa, lakini kwa hapa serikali haina utaratibu huo, ingawa tunaweza kulipokea wazo hili na kulifanyia kazi," alisema.

# Vijiji 70 vya Mkalama kupata umeme 2021

NAIBU Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amesema vijiji 70 vya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida vinatarajiwa kufikishiwa nishati ya umeme ifikapo Juni, 2021.

Mgalu aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Iramba Mashariki (CCM), Allan kiula, ambaye katika swali lake alisema Serikali inatekeleza mpango kabambe wa kusambaza umeme vijijini kupitia mpango wa REA.

Alihoji ni lini vijiji vyote 70 vya Wilaya ya Mkalama vitapata umeme wa REA II na kama ipo tayari kuweka umeme katika vitongoji vinavyopitiwa na njia ya umeme wa REA.

Akijibu, Naibu Waziri Mgalu alisema Serikali kupitia REA inatekeleza dhamira yake ya kufikisha umeme katika vijiji vyote nchini ifikapo Juni mwaka 2021 vikiwamo 70 vya Wilaya ya Mkalama. "Katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini awamu ya II jumla ya vijiji 14 vya Wilaya ya Mkalama vimewekwa kwenye mpango wa utekelezaji wa kupatiwa umeme kupitia Mkandarasi M/S JV EMEC & Dynamics," alisema. Hata hivyo, alisema hadi kufikia Aprili mwaka huu, vijiji vinne vya Ntiko Kanyantungu, Nkito Nkurui, Ibaga Sekondari na Ibaga Centre viliwashiwa umeme na wateja zaidi ya 100 wameunganishiwa umeme. "Kwa sasa mkandarasi anaendelea na kazi ya kuunganisha umeme katika vijiji 10 vilivyobaki ambapo kazi hiyo itakamilika ifikapo Juni mwaka huu," alisema.

Alisema vijiji na vitongoji vilivyopitiwa na miundombinu ya umeme katika Wilaya ya Mkalama vimejumuisha katika mpango wa kupatiwa umeme kupitia mradi wa ujazilizi awamu ya pili unaotarajiwa kuanza Julai mwaka huu. Aidha, alisema mradi huo utahusisha pia kuvipatia umeme vitongoji vyote vya Wilaya ya Mkalama vilivyopitiwa na njia za umeme kupitia utekelezaji wa mradi wa REA III mzunguko wa kwanza unaoendelea na utakamilika mwezi Juni mwaka 2020.

# Ahoji ununuzi hospitali wilaya

MBUNGE wa Kilindi (CCM), Omary Kigua, ameihoji serikali ni lini itainunua Hospitali ya Wilaya ya Kilindi inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Akiuliza swali bungeni jana, Kigua alisema kwa muda mrefu sasa wilaya hiyo haina hospitali, lakini wanayo Hospitali ya Rufani inayomilikiwa na kanisa hilo.

"Na watumishi wote na huduma zote za hospitali hii zinagharamiwa na Halmashauri ya wilaya na KKKT ni wamiliki wa majengo," alisema.

Akijibu, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Josephat Kandege, alisema mwaka 2010 serikali iliingia mkataba na kanisa hilo kwa lengo la kutumia majengo yake kwa ajili ya kutoa huduma za afya.

Alifafanua kuwa Hospitali hiyo Teule ya wilaya(DDH) ya Kilindi inahudumia wananchi wapatao 264,000.

"Serikali inatumia utaratibu huo ukiwa ni ushirikiano na taasisi binafsi yakiwamo mashirika ya dini pale ambapo hakuna hospitali ya wilaya," alisema.

Alieleza kuwa katika hospitali hiyo Serikali inalipa mishahara ya baadhi ya watumishi walioajiriwa na serikali na kupeleka fedha kwa ajili ya uendeshaji wa hospitali ambazo zinatumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Alibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2018/19 hospitali hiyo iliidhinishiwa Sh. milioni 153.6 kutoka Mfuko wa pamoja wa afya ambazo ni asilimia 25 ya fedha zote za mfuko kwa hospitali za wilaya.

Vilevile, alisema katika mwaka wa fedha 2019/20 hospitali hiyo imetengewa jumla ya Sh. milioni 153.6 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Hata hivyo, alisema Serikali haina mpango wa kununua Hospitali ya Wilaya ya Kilindi inayomilikiwa na KKKT kwa kuwa mpango wa serikali ni kuhakikisha kila halmashauri inakuwa na hospitali ya Serikali ngazi ya halmashauri.

Alisisitiza kuwa pale ambapo bado Serikali haijajenga itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kama inavyofanyika sasa.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# TTB yaagiza wadau utalii kuboresha miundombinu

**Na Cynthia Mwilolezi**

ARUSHA

MKURUGENZI Mtendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Devotha Mdachi, ameziagiza Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) kuboresha miundombinu katika maeneo yao ili kukidhi mahitaji ya kasi ya ongezeko la watalii mwaka huu.

Akizungumza jana wakati alipotembelea NCAA na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Mdachi alisema watalii kutoka nchi mbalimbali ikiwamo China wameanza kumiminika kutembelea vivutio vilivyopo na kuonyesha shauku ya kuendelea kuja kwa wingi.

Mdachi ambaye alikuwa ameongozana na watalii zaidi ya 300 toka China waliotembelea hifadhi hizo, alisema licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na mamlaka hizo na serikali, bado kuna changamoto ndogo ndogo zimejitokeza katika kuwahudumia wageni hao ikiwamo upungufu wa vyoo kwa baadhi ya maeneo.

"Watalii hawa wamefurahishwa sana kutembelea hifadhi zetu na katika mkataba wetu, tumekubaliana kuwa mpaka itakapofika Disemba mwaka huu wawe wameshatuletea jumla ya watalii 10 000," alisema.

Mdachi alisema licha ya kuhamasisha utalii China, pia wamejipanga kuhamisha utalii Urusi, India na nchi nyingine za Mashariki ya mbali ili waje kwa wingi kuona vivutio.

Aidha, aliwataka vijana waliosoma China ambao hawajapata ajira na ambao wanajua lugha ya kichina kuomba ajira kwa makampuni ya utalii nchini ili kuweka urahisi wa mawasiliano wageni hao wanapokuja nchini.

Mwenyekiti wa Bodi ya TTB, Jaji mstaafu Thomas Mihayo, alisema watalii hao wamevutiwa sana na vivutio vilivyopo nchini na kuahidi kuvitangaza katika maeneo mbalimbali nchini kwao.

Aidha alisema wameahidi kuwaleta wataalamu wa kutengeneza bustani maalum zenye ukubwa wa ekari sita kila moja zenye maua mbalimbali ya asili, kama ilivyo bustani moja nchini humo ambayo watalii wataona aina mbalimbali za maua na mimea ya asili.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akizungumza na waandishi wa habari kuwakaribisha wanahisa wa Benki ya CRDB katika mkutano mkuu wa wanahisa wa 24 utakaofanyika Mei 18, 2019, katika ukumbi wa AICC Jijini Arusha. Mkutano huo utatanguliwa na Semina ya wanahisa itakayofanyika kesho. Kulia ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Joseph Witts. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi wakumbushwa bidii kazini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru Dk. Wilson Mahera, amewakumbusha watumishi kufanya kazi kwa bidii na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma ili kuwapelekea wananchi maendeleo.

Akizungumza katika kikao kazi na watumishi wa halmashauri hiyo, Mahera, alisema jambo muhimu litakalosaidia kuleta maendeleo kwenye halmashauri hiyo ni watumishi kufanya kazi kwa kujituma na uwajibikaji wanapowahudumia wananchi.

Alisema watumishi wa umma wana jukumu la kuwahudumia wananchi bila kujali hali zao na itikadi zao za kisiasa kwa sababu ni haki ya kila mwananchi kupata huduma bora ambazo wanazihitaji na kwa kufanya hivyo, watawajengea imani wananchi kwa serikali inayowaongoza.

"Kila mwananchi ana haki ya kuhudumiwa na kupata huduma bora na sahihi anayohitaji bila kujali hali yake ya kiuchumi, itikadi za kidini na kisiasa," alisema Mahera.

Aidha, aliwataka wakuu wa idara na vitengo kuwasimamia watumishi walioko chini yao kuhakikisha wanatekeleza majukumu ya kusimamia miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na idara na vitengo.

"Nawataka wakuu wote wa idara na vitengo kuwajibika vizuri na kuhakikisha mnawasimamia watumishi walioko chini yenu vizuri, huku mkisimamia vyema miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya idara na vitengo vyenu, na kuacha tabia ya kupokea rushwa," alisema Mahera.

Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Arusha, Hamis Mpume, aliahidi kushirikiana na watumishi wa ngazi zote kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na kuleta maendeleo katika halmashauri yao.

Aliwataka watumishi wote kufanya kazi kwa ushirikiano kwa kuzingatia nidhamu ya kazi kwa kuwa ndicho kipaumbele cha uongozi uliotukuka.

# Serikali yawapa jukumu watalii

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, ameeleza kuwa Serikali itatumia watalii wanaokuja nchini kutembelea vivutio kutangaza fursa zilizopo za uwekezaji katika sekta ya utalii ,biashara na madini.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wawekezaji kutoka China, katika kongamano la uwekezaji lililofanyika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC) jijini hapa.

Kairuki alisema lengo la kongamano hilo ni kubadilishana mawazo na uzoefu katika eneo la uwekezaji pamoja na kutangaza fursa za kibiashara.

"Serikali ipo bega kwa bega na serikali ya China kujenga jamii yenye ushirikiano na maendeleo yetu na urafiki uliopo," alisema.

Alisema wanakaribisha maamuzi ya China kufungua milango kwa Tanzania katika kuwekeza kwa lengo la kulifikia soko lake kubwa katika sekta zote muhimu kuanzia katika uwekezaji upande wa utalii, biashara, madini na fedha.

"Napenda kuwahakikishia marafiki zangu wa China kuwa Tanzania ni ya amani... uwe na uhakika wa usalama wako binafsi, pia tupo tayari kukaribisha uwekezaji kutoka China na kuwahakikishia usalama wa mitaji yenu kwani tunazo sera nzuri na sheria thabiti," alisema Waziri Kairuki.

Alisema Tanzania ni mshirika anayetegemea mdau anaeaminika kama China, hivyo ndio sababu haikujali Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za kwanza za Afrika kuhusishwa katika mpango wa ukanda mmoja wa kibiashara (One Belt One Road Initiative) kwa sababu Tanzania ni miongoni mwa nchi nne vinara chini ya mpango wa uzalishaji na uwezeshaji wa pamoja wa China.

Amewataka Watanzania kuitangaza vizuri nchi hususan kipindi hiki ambacho watalii wanakuja kutembelea vivutio mbalimbali nchini, huku akiwataka waandishi wa habari kuona umuhimu wa kuitangaza nchi yao kama waandishi kutoka China wanavyofanya.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Geoffey Mwambe, alisema kongamano hilo litasaidia ukuaji wa uchumi na wao wamejipanga kikamilifu kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini, ambazo sasa zimefunguka kwa wingi.

Jumla ya wawekezaji 50 kutoka kampuni 25 wameshiriki kongamano hilo ambapo pia watalii 336 kutoka China 336 watapata fursa ya kutembelea vivutio vya utalii ikiwamo Hifadhi ya Ngorongoro.



Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (katikati), akikabidhi funguo ya gari aina ya Toyota Pick Up Double Cabin, kwa Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, kwa ajili ya kusaidia shughuli za uchaguzi ujao wa serikali za mitaa katika Jimbo la Hai. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Kampuni za uzalishaji kuku Uholanzi kufundisha nchini

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAWEKEZAJI wa kampuni saba za uzalishaji wa kuku wa nyama na mayai kutoka nchini Uholanzi, wameingia makubaliano na Serikali ya Tanzania kutoa mafunzo na vifaa vya ufugaji kuku bora wa kisasa katika mikoa ya kanda ya Kaskazini ili kuwezesha wafugaji wadogo kufuga kuku kibiashara.

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo yaliyofanywa na mabalozi wa nchi hizo mbili katika Chuo cha Kilimo na Mifugo Kilacha, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema kwa sasa makubaliano hayo yatalenga utoaji wa vifaa vya mafunzo kwa wafugaji wa kuku hapa nchini.

Alisema umefika wakati sasa kwa wafugaji kuzalisha kuku wa nyama na mayai kwa njia ya kisasa na kutumia fursa hiyo kutoka kwa wawekezaji nchini Uholanzi kupata mbinu bora za kisasa za ufugaji wa kuku zitakazowezesha kuongeza kipato na lishe katika familia zao.

"Makubaliano hayo tuliyoyaingia leo (jana) kati ya nchi hizi mbili yana uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko katika jamii ya Watanzania kwa kuongeza kipato na lishe bora...tunawaomba Watanzania kujitokeza katika kuchangamkia fursa hii ili kutokomeza tatizo la ajira nchini kwa kujiajiri," alisema Dk Anna.

Kwa upande wake Balozi wa Tanzania nchini Uholanzi, Irene Kasyanju na Mkurugenzi wa taasisi ya maendeleo na biashara katika sekta ya kilimo nchini Uholanzi, Mackenzie Masaki, wamesema wawekezaji hao watafundisha wafugaji kufuga kisasa kuanzia katika ujenzi wa mabanda, chakula bora, machinjio na masoko ya kuku na mayai.

"Mafunzo tutakayotoa ni lazima tuanzie katika ujenzi wa mabanda, namna ya kuandaa chakula bora na jinsi ya kuwalisha na masoko ya bidhaa watakazozalisha, "alisema Msaki.

Nao baadhi ya wafugaji na wadau wa uzalishaji wa pembejeo za mifugo Tanzania, Shanel Ngowi, alisema kwa sasa sekta hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo uingizwaji wa pembejeo bandia na kusababishia wafugaji kupata hasara na baadhi waliochukua mikopo katika taasisi za kifedha kushindwa kurejesha.

# Madereva waeleza sababu kuyumba kwa umoja wao

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

BAADHI ya wanachama wa chama cha madereva wa usafirishaji abiria wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro, wamesema kutoitishwa kwa mikutano pamoja na kusomewa taarifa za mapato na matumizi ni moja ya sababu kubwa ya madereva hao kujitoa na kuachana na chama hicho.

Kufuatia hali hiyo, madereva hao wameiomba serikali wilayani humo kutuma wakaguzi wa ndani wa halmashauri hiyo ili iweze kukagua mahesabu ya mapato na matumizi ambayo hayajasomwa kwa wakulima kuanzia mwaka 2017.

Wakizungumza katika mkutano wa dharura uliofanyika stendi ya mabasi wilayani humo huo mbele ya viongozi Gilbeti Kileo na Jackoson Kwayu,

walisema kuwa madereva hao walitarajia mikutano hiyo ingetoa hali halisi ya mapato na matumizi yanayotokana na ukusaanywaji wa fedha zinazotoka katika kituo cha mabasi cha Naibili, Karansi, Ngarenairobi na kituo cha Sanya Mjini.

"Katika chama chetu tulikubaliana tusomewe mapato na matumizi, lakini viongozi wetu hawafanyi hivyo hali ambayo inafanya madereva hao kujitoa na kuachana na chama hicho," alisema Kileo na kuongeza: "Hiki chama kilianzishwa kwa ajili ya kusaidiana madereva katika shughuli mbalimbali, lakini imekuwa tofauti kikinufaisha watu wachache," alisema Kileo.

Kila baada ya miezi sita tulikubaliana kila mtu apewe 100,000, lakini toka nijiunge sijapata fedha hiyo.

Mwenyekiti wa chama hicho, Frank Moshi, alisema hakuna dereva anayelazimishwa kutoa Sh. 1000 kwa kila safari kama sio mwanachama wa chama hicho, lakini anayetoa anatoa kwa hiyari yake, kuhusu mapato na matumizi yanasomwa kwa mwezi mara mbili.

Alisema anayedai kuwa hayasomwi atakuwa sio mwanachama .

Mkuu wa Wilaya hiyo Onesmo Buswelu baada ya kusikiliza kero zao alibaini kuwa utaratibu wa ukusanywaji wa fedha hizo haujakaa vizuri kwa kuwa mkusanyaji anakusanya fedha na kukabidhi bila maandishi hali ambayo kiutaratibu haipo.

Buswelu aliongeza kuwa wanachokifanya ni kuhakikisha kama kuna fedha ya wananchi inapotea wao kama serikali lazima waifuatilie ili kuboresha chama hicho .

"Kama kuna mtu aliyetafuna fedha ya wanachama hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yake," alisema Buswelu.

Buswelu aliongeza kuwa kufuatia hali hiyo Mei 19, mwaka huu, amewataka viongozi wa chama hicho, madereva wote wakiwamo wanachama na wasio wanachama kukutana naye kwa lengo la kushughulikia masuala hayo.

# TRA yahamasisha ulipaji kodi majengo

**Na Paul William,** MOSHI

MAMLAKA ya Mapato nchini (TRA), Mkoa wa Kilimanjaro imewaasa wananchi wanaomiliki nyumba kujijengea tabia ya kulipa kodi za majengo ili kusukuma mbele maendeleo ya taifa.

Kaimu Ofisa Huduma na Elimu kwa mlipakodi, Mkoa wa Kilimanjaro, Hashim Amani, alitoa hamasa hiyo katika maadhimisho ya wiki ya elimu kwa mlipakodi yaliyofanyika katika viwanja vya Posta.

Amani alisema, kwa sasa kumekuwapo na mwitikio mkubwa kwa wananchi kulipa kodi za majengo baada ya kutambua umuhimu wa kodi kwa maendeleo ya taifa pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na mamlaka hiyo katika kutoa elimu kwa wananchi.

Alisema, kwa mujibu wa takwimu, wakati mamlaka hiyo ikikabidhiwa ukusanyaji wa kodi za majengo Manispaa ya Moshi ilikuwa imeshasajili nyumba 12,000, lakini kwa kipindi cha miaka miwili mamlaka hiyo imesajili nyumba 14,000.

"Wiki ya elimu na huduma kwa mlipakodi, maofisa wa TRA hutoka ofisini na kuwafuata walipakodi kwa ukaribu zaidi na kusikiliza kero mbalimbali za ulipaji kodi pamoja na kutoa huduma kwa kodi mbalimbali ikiwamo usajili wa majengo," alisema Amani.

Ofisa Huduma huyo alisema kuwa, kodi ndio damu au injini ya taifa na kwamba bila kodi barabara, huduma za afya, elimu na nyingine zitashindwa kuendelea.

Alisema wiki hii wanategemea kutembelea masoko ya Sadala, lililopo wilayani Hai na Mwanga ili kuwahamasisha wananchi kutambua umuhimu wa ulipaji wa kodi.

Alitoa wito kwa wananchi kutambua umuhimu wa ulipaji kodi ili kusaidia maendeleo ya nchi kusonga mbele na kuongeza kuwa kodi haina itikadi za vyama na hiyo ni kutokana na makusanyo hayo kusaidia Watanzania.

Wakizungumzia wiki hiyo wananchi waliojitokeza katika viwanja hivyo vya Posta waliipongeza serikali kupitia Mamlaka ya Mapato kwa kutambua umuhimu wa kutenga wiki hiyo ili waweze kuuliza maswali yao yahusuyo kodi.

# ama

ALHAMISI MEI 16, 2019

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 17

**Tabu iliyoko kwa kichaa cha mbwa**



Ukurasa 14

SHINYANGA KATIKA BIMA ILIYOBORESHWA TENA



Ukurasa 16

**Kuendekeza mila kunavyowabebesha mimba wanafunzi wilayani Kishapu**



## BALAA YA MVUA DAR

# Mjimwema Kigamboni kulivyofurika kona zote

Ukurasa 18

# Wafuta sheria inayoruhusu utoaji mimba

**ALABAMA,** Marekani

SERIKALI katika jimbo la Alabama nchini hapa, limepitisha sheria inayopiga marufuku utoaji mimba kwa namna yoyote. Kabla ya hapo, tendo hilo lilikuwa ruksa kisheria.

Kwa mujibu wa sheria huyo, marufuku ya utoaji mimba hizo unajumuisha hata kama waliopeana mimba wana ukaribu wa kindugu na wameshiriki tendo hilo au mwanamke alibakwa

Hata hivyo, upitishaji wa sheria hiyo 'mbichi' tayari inakabiliwa na maombi kinzani wasiokubalina nayo wanadai wataenda mahakamani kuipinga, ili kuendeleza ruksa ya kisheria jimboni humo, iliyokuwamo tangu mwaka 1973.

Serikali nayo tangu kupitishwa sheria, imeweka msimamo kwamba itapambana kuitetea iwapo kutakuwapo pingamizi dhidi ya uamuzi wake.

Kama ilivyo Alabama, kuna majimbo mengine 16 ya nchi hiyo, yanayoelezwa kuwa mbioni kupitisha sheria ya marufuku kama hiyo.

Nchini Marekani, sheria nyingi kubwa zinasimamiwa katika msingi ya majimbo

Mapema mwaka huu, Mahakama Kuu nchini Marekani ilizuia utekelezaji wa sheria moja inayopinga kutoa mimba jimboni Louisiana, wakati ikiendelea kusikiliza shauri lililofunguliwa .



Seneta wa Chama cha Democratic, aking'aka kupinga sheria hiyo. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# SHINYANGA KATIKA BIMA ILIYOBORESHWA TENA

## • Malengo safi, mafanikio hayajafika robo • Manispaa juu; Msalala, Shy Vijijini mkiani • Watoto 200 mazingira magumu watabasamu • Wanufaika wamwaga sifa zenye ushahidi



Mzee Mohamed Mkumbola, mkazi wa Manispaa ya Shinyanga, akitoa shukrani kwa serikali kuwakatia bure wazee wasiojiweza kadi ya Bima ya Afya ya Jamii, CHF. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU**

**Na Marco Maduhu,** Shinyanga

NCHINI Tanzania, suala la huduma za watu kutibiwa kupitia mifuko ya bima za afya si ngeni. Katika huduma hizo, iko Bima ya Afya ya Jamii iitwayo CHF, inayotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

CHF ilianzishwa kwa madhumuni ya kusaidia upatikanaji matibabu kwa gharama nafuu, hususani kaya zenye kipato cha chini zinazokosa matibabu, ili wapatiwe bure na kuokoa afya zao.

Utekelezaji wa bima hiyo uliboreshwa katika baadhi ya maeneo nchini, ikiwamo Manispaa ya Shinyanga. Ulianza Februari mwaka 2016 kwa ushirikiano na mradi uitwao HPSS (Tuimarishe Afya).

> **"Mikakati ambayo tumejiwekea 2019 ni kutoa elimu kwa wananchi kujiunga na bima hii ya afya CHF iliyoboreshwa.**

Lengo kuu lililopo, ni kutoa huduma na kuokoa maisha ya wenye kipato cha chini, wanapougua ghafla na hawana pesa za matibabu.

Kati ya mwaka 2016 na 2018, gharama za kujiunga na bima ya CHF ziliongezwa. Ilikuwa Sh. 10,000 kwa kaya ya mtu mmoja inayojumuisha wanufaika sita na kufikia 30,000, zikiendana na maboresho ya huduma.

Hapo inahusisha watu sita katika kaya na inajumuisha baadhi ya hospitali binafsi, zinapokea kadi hizo

Wananchi waliweza kupata huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati, kituo cha afya na hospitali za wilaya na mkoa. Hiyo ilikuwa katika mikoa mitatu ya Shinyanga, Morogoro na Dodoma.

### MRATIBU NHIF

Mratibu wa CHF iliyoboreshwa katika Manispaa ya Shinyanga, Octaviani Kiwone, anasema jamii haina uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa kujiunga na bima, hiyo ambayo ni mkombozi wa afya za wananchi wa kipato cha chini.

Anasema, CHF kwa kiwango kikubwa inahusika na wananchi wa kipato cha chini, wanaoendelea kutoa elimu ya kuhamasisha wajiunge, ili watibiwe hasa katika vipindi wanapougua.

"Katika Manispaa ya Shinyanga, tulipewa lengo la kuunga kaya 33,623 kwenye bima ya CHF kwa muda wa miaka mitatu kuanzia 2016 hadi 2019), lakini mpaka sasa tumeunga kaya 7, 871,: anasema Kiwaone na kufafanua:

"Ni sawa na asilimia 23.4 idadi ambayo ni ndogo na kunahitajika jitihada zaidi za hamasa, kaya nyingi zipate kujiunga.

"Mikakati ambayo tumejiwekea kwa mwaka huu (2019) ni kutoa elimu kwa wananchi kujiunga na bima hii ya afya CHF iliyoboreshwa, kwa kutembelea kwenye masoko, stendi za mabasi, minadani, vijiwe vya bodaboda, viwandani na kwenye nyumba za ibada."

Anasema, pia wakiboresha utoaji wa huduma kwa wagonjwa wenye kadi hizo, matibabu na dawa, manispaa ikizilipa fedha vituo vya afya kwa wakati, lengo ni kuwasaidia wananchi kulinda afya zao.

### WANUFAIKA WAFUNGUKA

Aidha, baadhi ya watu ambao ni wakazi wa manispaa ya Shinyanga, wametoa ushuhuda wa ufanisi wa bima hiyo iliyoboreshwa na kusaidia kuokoa maisha yao, walipopatwa na majanga ya maradhi.

Venat Lyamukama, ni mkazi wa Kata ya Kambarage katika Manispaa ya Shinyanga, ambaye ni miongoni mwa wanufaika wenye kadi za CHF iliyoboreshwa, anakiri kwamba imemsaidia matibabu yake na familia, yenye watu wegine watano.

Anasema, ni kadi yenye historia ya kumsaidia katika umri wake mkubwa anaohitaji matibabu ya kila mara ili kukoa uhai wa mkewe aliyelazwa hivi karibuni katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga.

"Nilikata kadi hii ya Bima ya Afya ya Jamii, iliyoboreshwa mwaka jana. Mara baada ya kuhamasishwa na kupewa elimu juu ya umuhimu wake, nikaona ngoja niikate ili nione kama kweli ina faida, sababu tulikuwa tukisikia mtu mwenye bima hapewi matibabu vizuri kama yule mwenye pesa mkononi," anasema Lyamukama.

"Nilipoikata nikajaribu kuitumia kama kweli nitapewa huduma mbovu, lakini matarajio yakawa tofauti, nikapewa matibabu mazuri pamoja na madawa bila ya kutoa hata Shilingi,"anaongeza Lyamukama.

Mnufaika mwingine wa CHF iliyoboreshwa, Sophia Juma, anayejitambulisha anaishi na shangazi yake na hana uwezo kifedha, wanachanga fedha wapate kadi hiyo.

Anakiri, imekuwa msaada mkubwa kwao kupatiwa matibabu pasipo kuwagharimu chochote, zaidi ya usafiri wa kwenda hospitali. Sophia anafafanua zaidi:

"Naipongeza sana serikali kuan-

AFYA

# SHINYANGA KATIKA BIMA ILIYOBORESHWA TENA

zisha mfuko huu wa Bima ya Afya ya Jamii CHF, kwa kupatiwa matibabu kwa gharama nafuu ya Sh. 30,000 kwa mwaka mzima, bila ya kujali unaumwa ugonjwa wa aina gani, jambo ambalo ni jema sana, hasa kwetu sisi wananchi wa hali ya chini."



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, akimkabidhi kadi ya Bima ya Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa, Regina Kulwa, mkazi wa Kambarage mjini Shinyanga, alipozuru mwaka jana kuhamasisha wananchi kujiunga. **PICHA ZOTE: VERONICA ROMWALD.**

### KATIBU TAWALA

Boniphace Nchambi, ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Shinyanga, b anatoa wito wananchi wajiunge na mfuko wa CHF iliyoboreshwa, ambayo itakuwa msaada mkubwa kwa matibabu na kuokoa afya zao.

Pia, anayataka mashirika yanayotoa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, wakiwamo yatima, kwanba wawakatie kadi hizo za bima ya afya kuwahakikishia ulinzi wa afya zao wanakapougua.

"Watu wamekuwa wakipuuzia kukata bima hii ya afya ya jamii CHF, lakini siku ukiugua na kukutwa huna pesa ya matibabu, ndipo utajua umuhimu wake. Hivyo, nawaomba wananchi waikate na siyo kusubiri mpaka wapate shida na kuanza kuja kuomba msaada kwenye ofisi za serikali,' anasema Nchambi.

### MGANGA MFAWIDHI

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Kambarage Shinyanga Mjini, Daniel Nsaningu, anapongeza utoaji wa matibabu kupitia bima ya a CHF, akisema imekuwa msaada mkubwa kwenye kituo hicho, kwa upatikanaji dawa za kutosha kuliko utoaji fedha mkononi.

Anasema katika CHF, serikali imekuwa na mchango mkunbwa kwa kuendelea kuboresha huduma za afya, ikiwamo ujenzi wa majengo, dawa na vifaa tiba.

"Utoaji huduma ya matibabu kupitia CHF, imekuwa msaada mkubwa sana wa utoaji wa tiba sahihi, kwa wananchi. Tumekuwa na dawa za kutosha, kuliko hapo zamani na hakuna malalamiko tena kwa wagonjwa kuhusu ukosefu wa dawa,"anasema Dk. Nsaningu.

### MRATIBU 'TUIMARISHE AFYA'

John Richard, ni Mratibu wa HPSS (Tuimarishe Afya) Shinyanga, ambao ni wasimamizi wa CHF iliyoboreshwa kwenye halmashauri, anasema lengo ni kuokoa afya za wananchi wa kipato cha chini wapatiwe matibabu kwa gharama nafuu, kwa bei ya Sh. 30,000 kwa mwaka.

Richard anasema, suala la uhamasishaji wananchi kujiunga kwenye bima hiyo inayotajwa, Manispaa ya Shinyanga ndiyo inayoongoza kufanya vizuri ikiwa na asilimia 23.4, inafuatiwa na Mji Kahama (19%); Ushetu (10%); Kishapu (9.7%), Msalala (7.5%) na Shinyanga Vijijini (7.5%).

Anazitaka halmashauri kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa wananchi, ili wajiunge na CHF iliyoboreshwa, ili wapate matibabu ya bure kuokoa afya zao, hasa watakapopatwa na magonjwa, bila ya kuwa na fedha.

> "Watu wamekuwa wakipuuzia kukata bima hii ya afya ya jamii CHF, lakini siku ukiugua na kukutwa huna pesa ya matibabu, ndipo utajua umuhimu wake.



Ofisa Uandikishaji wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) katika Manispaa ya Shinyanga, Jackson Njau, akiingiza taarifa za wananchi waliojitokeza kukata bima hiyo.

### MKURUGENZI TVMC

Mkurugenzi wa shirika la TVMC, Mussa Ngangala, wanaojihusisha na kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu, Shinyanga Mjini, anasema wamekuwa na kawaida ya kusaidia watoto kwa kuwakatia kadi ya CHF iliyoboreshwa, kuwarahisishia matibabu.

Anasema mwaka jana, 2018, aliwakatia watoto 200 wanaoishi katika mazingira magumu kutoka kwenye kata za Chamaguha, Ibadakuli, Kizumbi, Mwawaza na Mwamalili, ambao wazazi wao hawana uwezo mzuri kifedha na wamekuwa wakisumbuka kupata matibabu pale wanapougua.

"Kwenye mradi wetu wa kuzuia mimba na ndoa za utotoni, tumeona tuweke na kitengo cha kuwakatia bima za afya ya CHF iliyoboreshwa watoto hawa ambao wanaishi katika mazingira magumu, ili wanapougua na kukosa pesa za matibabu, wasiweze kurubunika na kuingia kwenye vishawishi," anasema Ngangala.

"Zoezi hili la ukataji bima za afya kwa watoto hawa, ni endelevu. Imekuwa msaada mkubwa sana kwao katika kuimarisha afya zao, pamoja na wazazi wao, ikiwa kwenye kaya moja wanatibiwa watu sita kwa mwaka mzima," anaongeza.

AFYA

# Kuendekeza mila kunavyowabebesha mimba wanafunzi wilayani Kishapu

## • Serikali yawanasa, nao 'wajichomoa' • Harusi zinafungwa kupitia 'mke feki' • Imani yao binti kwa wazazi haaminiki

**Na Marco Maduhu,** Kishapu

TATIZO la wanafunzi kupewa ujauzito na kuolewa ndoa za utotoni wilayani Kishapu na kisha kukatishwa masomo yao, limeendelea kuwa kero kutokana na wazazi wao kuendekeza masuala ya mila na desturi kandamizi zilizopitwa na wakati, kwa kutopenda kusomesha watoto wa kike.

Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, inakabiliwa sana na tatizo la wanafunzi wa kike kupewa ujauzito na kukatishwa masomo yao, wengine kuolewa ndoa za utotoni.

Takwimu za mwaka jana zinajumlisha wanafunzi 59 wa shule za Sekondari wilayani humo, walikatishwa masomo kwa sababu ya ujauzito na baadhi yao kuolewa ndoa za utotoni.

Takwimu za mwaka huu 2019, kuanzia Januari hadi Machi, tayari kuna wanafunzi 10 waliokwishapewa ujauzito na kuacha masomo.

### DC KISHAPU

Nyabaganga Taraba, ni Mkuu wa Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, amekuwa akipambana kutokomeza tatizo hilo la wanafunzi kukatishwa masomo kwa sababu ya ujauzito na wengine kuolewa ndoa za utotoni ili wanafunzi hao watimize ndoto zao.

Anasema katika mapambano hayo, amekuwa akikutana na kikwazo cha wazazi kuendekeza mila na desturi kandamizi zilizokwishapitwa na wakati, hawapendi kusomesha mabinti zao, kwa madai kwamba ni watu wa kuolewa tu na kuleta mali ya mifugo nyumbani.

Taraba anaeleza kuwa, serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, likiwamo Shirika la Save The Children, wamekuwa wakijitahidi kutoa elimu ya kubadilisha mtazamo ya wananchi kuachana na mila hizo, lakini hali bado ni ngumu, mimba za wanafunzi na ndoa za utotoni zinaendelea kuwapo.

"Sisi kama serikali wilayani Kishapu, tumekuwa tukipiga sana vita vitendo hivi vya wanafunzi kupewa ujauzito na kuolewa ndoa za utotoni.

"Nawataka watuhumiwa kuwafikisha mahakamani, lakini jamii yenyewe imekuwa ikikumbatia matukio haya na hata kutofika mahakamani na hatimaye kesi kufutwa," anasema Taraba.

"Nawaombeni wana- Kishapu tubadilike, tuachane na masuala haya ya mila na desturi kandamizi, tusomeshe watoto wetu wa kike bila ya ubaguzi," anasema mkuu wa wilaya huku akiwaasa wanaume kuacha kuwasumbua mabinti wanafunzi kwa mapenzi, ili kuwaacha watimize malengo, huku taifa likipata wasomi.

Anatumia wasaa huo kuwainua viongozi wa serikali vijijini, katika kata na walimu, kuacha tabia ya kupokea 'vitu vidogo' vinavyosaidia kuharibu ushahidi wa kesi za mimba za wanafunzi, kwa kisingizio 'alikuwa hasomi.'

Mkuu wa wilaya anahimiza kuwapo nguvu za pamoja, kutokomeza matukio hayo, kunajenga njia bora ya mafanikio.

Tahadhari yake kwa watumishi wa umma ni kwamba: "Mtumishi yeyote wa serikali ambaye atabainika kushiriki kwenye tuhuma hizi za kuharibu kesi za mimba za wanafunzi, pamoja na kushiriki kwenye harusi za ndoa ya utotoni 'nitakula naye sahani moja' sababu taarifa zenu ninazo."



Wanawake wa Kishapu kwenye tamasha la Mwanaume Jasiri, linalopinga mimba na ndoa za utotoni kwa mabinti. **PICHA ZOTE NA MPIGAPICHA WETU**

> **Mwaka huu kwenye Kata yangu hii ya Shanghihilu tayari wanafunzi wanne wameshapewa ujauzito na kuacha masomo.**



Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyabaganga Taraba, akiwakemea wanaume wilayani kwake wanaoendekeza mila na desturi za kuozesha mabinti ndoa za utotoni.



Meneja Mradi wa kutokomeza mila na desturi kandamizi, Merry Kyando, kutoka Shirika la Save The Children, akielezea majukumu ya mradi wake.



Mzee Bagwani Omari, ambaye mkazi wa wilayani Kishapu akizungumza.

### OFISA MAENDELEO JAMII

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Rehema Edson, anataja takwimu za wanafunzi kuwa mwaka jana wanafunzi waliokatishwa masomo kwa sababu ya ujauzito wako 59 na mwaka huu, hadi Machi, walishakuwepo wanafunzi 10.

Anasema, serikali kwa kushirikiana na wadau, wametoa elimu kwa wazazi wapende kuwasomesha mabinti zao, kuwatimizia mahitaji na wasiwaozeshe, ingawa katika hilo wameendelea kuwa wagumu kubadili fikra zao.

"Imefikia mahali sasa tunashindwa kuelewa nini hasa tatizo la wanafunzi kuendelea kupewa ujauzito na wengine kuolewa ndoa za utotoni, kwa sababu kama elimu tumetoa ya kutosha na tunaendelea kuitoa, lakini tatizo bado liko palepale,"analalamika Rehema.

### MWENYE MILA

Bagwani Omari, ni mzee anayeishi wilayani Kishapu, akisema tatizo la wazazi kutopenda kusomesha mabinti zao, ni suala kongwe katika mila, hivyo ni mtihani mgumu kuliacha haraka.

Anarejea zama hizo, msichana hakuthaminika, bali alifanywa kitega uchumi cha familia. Alipokuwa, wazazi walianza kumtafutia mwenza wa kumuoa, ili familia inufaike pate na nyongeza ya mifugo na sifa ya utajiri wa ng'ombe.

"Familia ikizaa mtoto wa kike tu, inaanza kuishi kwa wasiwasi kuogopa aibu ndani ya jamii, endapo mtoto atapewa ujauzito akiwa bado nyumbani. Ndiyo maana, akishavunja ungo tu, lazima aolewe bila ya kujali yupo shule, kwa kutolewa mahari inayoanzia ng'ombe 25 hadi 50."

"Hivyo, tatizo hili la wanafunzi kupewa ujauzito na kuolewa ndoa za utotoni, haliwezi kwisha kwa haraka, sababu lipo kwenye damu za watu kwa kurithi kutoka kwa mababu zao.

"Kunahitajika elimu zaidi, pamoja na kuwafunga jela watuhumiwa, ndipo kidogo wataogopa kuendekeza vitendo hivi," anasisitiza Mzee Omari.

### MTENDAJI KATA

Yona Wiliam, ni Kaimu Mtendaji Kata ya Shangihilu wilayani Kishapu. Hiyo ni moja ya maeneo ambayo wanafunzi wanapewa ujauzito na kuolewa kwa wingi na ni tatizo kubwa la jamii, mzizi mkuu ni kuendekeza mila na desturi kandamizi, jambo linalowaumiza kichwa kumaliza changamoto zao.

Anasema, baada ya serikali kuwabana wazazi ambao wamekuwa wakiozesha wanafunzi ndoa za utotoni, kwa kuharibu ndoa hizo siku ya harusi wakiwa na Polisi, jamii.

Kutokana na hilo, sasa imebuniwa njia mbadala ya kubuni mbinu mpya ya kufungisha ndoa feki ya mtu mzima, kumbe harusi hiyo ni ya mtoto aliye na umri chini ya miaka 18.

"Mkuu wa wilaya alichokisema ni kweli kuna baadhi ya viongozi wenzetu wa vijiji wamekuwa wakishiriki kwenye harusi hizo za ndoa za utotoni kwa kupewa vitu vidogo, lakini kwa sasa tuna kabiliwa na changamoto nyingine ya kufungwa ndoa feki, ambapo mwanamke anayefungua ndoa hiyo siyo yeye, bali bibi harusi kafichwa ambaye ni mtoto,"anasema Wiliamu.

"Mwaka huu kwenye Kata yangu hii ya Shanghihilu tayari wanafunzi wanne wameshapewa ujauzito na kuacha masomo," anasema Mtendaji Kata na kuongeza:

"Tulipojaribu kufuatilia ilikuwa wafungishwe harusi, lakini baada ya kuona serikali imekuwa wakali, familia hizo za wahanga waliwasiliana na watuhumiwa na kisha kutoroka kusikojulikana."

Anaeleza kwamba, kutokana na jamii kuendekeza mila na desturi zilizopitwa na wakati, bado wanaendelea kutoa elimu kwa jamii kuachana na vitendo hivyo vya kuwapa mimba wanafunzi na kuwaozesha ndoa za utotoni.

Mtendaji Kata huyo, anasema kampeni hizo zinafanyika kupitia kwenye mikutano ya hadhara na vikao vya wazazi shuleni.

### MENEJA MRADI

Merry Kyando, ni Meneja wa Mradi wa Kutokomeza Mila na Desturi Kandamizi zilizopitwa na wakati, kutoka shirika la Save The Children mkoani Shinyanga, katika mradi wa miaka miwili unaolenga kuzifikia Kata 12 na wanaume 300 wilayani Kishapu.

> **Nawataka watuhumiwa kuwafikisha mahakamani, lakini jamii yenyewe imekuwa ikikumbatia matukio haya na hata kutofika mahakamani na hatimaye kesi kufutwa.**

Anasema lengo la mradi ni kuipatia jamii elimu kuachana na mila na desturi zilizopitwa na wakati za kutopenda kuwasomesha wasichana, pia kuwaozesha ndoa za utotoni, mambo yanayoonekana tatizo kubwa kwa wanafunzi na wazazi wa Shinyanga .

"Tumeanzisha mradi huu mara baada ya kufanya uchuguzi na kugundua tatizo ambalo limekuwa likisababisha kuendelea kuwapo matukio haya ya wanafunzi, kupewa ujauzito na kuozeshwa ndoa za utotoni. Ni mila na desturi ndipo tukaona ni vyema tuanze na utoaji wa elimu ya kutokomeza mila hizi," anasema.

Anasema, serikali na wadau wa maendeleo wasipotokomeza vitendo, hivyo taifa kuna hatari ya kuongozwa na wasiokuwa na upeo mzuri wa kielimu, kwa jinsia ya kike, hatimaye ni taifa kutumbukia katika umaskini.

### MWANAHARAKATI

Clement Benard, ni mwanaume aliyejengewa uwezo na Shirika la

INAENDELEA UK.20

## Tabu iliyoko kwa kichaa cha mbwa

HASA, kichaa cha mbwa ni nini? Inaelezwa kuwa ugonjwa hatari unaoathiri ubongo na kwa kawaida usipowahiwa kimatibabu, aliyeambukizwa anapoteza maisha.

Ikirejewa tena, cha kujuuliza, chanzo chake nini? Hilo ni ambukizo la virusi vinavyosababisha uvimbe wa ubongo, vinavyomtokea binadamu, mnyama au ndege.

Lakini, ni mara chache kuwapata wanyama wala majani na maambukizo kutoka mtu mgonjwa kwenda mwingine, ni mara chache sana.

Asilimia 99 ya watu huambukizwa na mbwa. Pia, maradhi hayo yanayowatokea wanyama kama vile paka, mbweha na mbwa mwitu.

Maambukizo ya maradhi hayo hupitia mate na damu, hasa kwa kung'atwa na mnyama anayeumwa. Ni mate kutoka kwa mnyama aliyeambukizwa yanayoweza kusambaza kichaa cha mbwa, hasa yanapokutana na utando telezi wa mnyama mwingine au binadamu.



Huduma ya tiba na kinga dhidi ya kichaa cha mbwa ikiendelea. **PICHA: MTANDAO**

### DALILI ZAKE

Ugonjwa hugundulika, baada ya dalili kuonekana, ikijumuishwa na homa kali. Hilo linafuatwa na dalili kama:Kukasirika au kuogopa ghafla; kuyaogopa maji; kukosa uwezo wa kutawala mwendo wa viungo vya mwili; na kupoteza fahamu.

Inaelezwa, mara dalili hizo zinapoonekana, maana yake ugonjwa umeshaanza kuharibu ubongo na mishipa midogo, hatua ya mwisho ikiwa ni kifo cha mgonjwa.

Muda kati ya kuambukizwa ugonjwa na mwanzo wa dalili, kawaida huchukua wastani wa mwezi mmoja hadi mitatu.

Hata hivyo, kipindi hicho kinaweza kutofautiana, ikazidi kufikia mwaka au kwa wiki kadhaa chini ya mwezi mmoja. Sababu kuu ni namna virusi lazima kusafiri vinavyosafiri kufikia mfumo mkuu wa 'neva.'

### TIBA NA KINGA

Watu wanaotibiwa mara moja baada ya kuambukizwa wanaweza kupona. Lakini, tiba inahitaji kutekelezwa kabla ya virusi havijaifikia ubongo.

Ni kawaida katika nchi nyingi, wanyama wengi hupewa chanjo za kujikinga ili wawe salama dhidi ya ugonjwa huo.

Kudhibiti wanyama na mipango ya chanjo zinapunguza hatari ya kichaa cha mbwa katika nchi kadhaa na kuchanja watu, kulipendekezwa kwa walio na hatari kubwa.

Kina nani wako hatarini?

Hapo kunatajwa kundi la wanaofanya kazi na watumia muda mrefu katika maeneo ambayo kichaa mbwa ni kawaida.

Inashauriwa kuosha mahali panapoumwa na mchukubo kwa dakika 15, kwa kutumia sabuni na nyenzo nyingime za usafi kuua virusi vya kichaa cha mbwa.

Inaelezwa, asilimia 95 ya vifo hivyo hutokea katika Bara Asia na Afrika. Hadi sasa inaelezwa maradhi hayo yako katika nchi zaidi ya 150 duniani.

MAZINGIRA

BALAA YA MVUA DAR

# Mjimwema Kigamboni kuli

- Ni mtindo, kila msimu wapo wanaohama
- Walia kufika kona zote, majibu 'sifuri'





Picha zinazoonyesha mandhari ya makazi ya Mji Mwema Ungindoni, Kigamboni, katika msimu wa mvua unaoendelea Dar es Salaam. Imekuwa hali ya kudumu mahali hapo kila mvua kubwa zinaponyesha. **PICHA ZOTE: ENOCK CHARLES.**

**Na Enock Charles**

HALI ya hewa ya Dar es Salaam, imebadilika sana, tena kwa hatua kubwa ndani ya muda mfupi. Iwapo mtu si mwenyeji wa jiji hilo, itakuwa vigumu kwake kuamini ushuhuda huo.

Joto na jua kali lililozoeleka kwa miezi kadhaa, limetoweka ghafla, mara kuwa ni mwelekeo wa baridi na mvua kubwa, kuizidi rekodi ya miaka mingi iliyopita.

Wakati mvua zilipoanza, umma ulifurahia kupungua joto, vumbi na kupatikana kwa yatokanayo na mvua zinazoendelea kama vile maji ya bure. Katika sura ya pili, katika baadhi ya maeneo na hasa mabondeni, si habari njema.

Bonde la Jangwani, ambalo ndilo linakusanya maji kuelekea baharini, limefurika mno. Kwa mara kadhaa mamlaka za kiserikali zililazimika kuchukua hatua ya kufunga barabara kati ya eneo la Magomeni na Faya.

Polisi nao, mbali na tahadhari za usalama kwa umma, imetangaza vifo vya watu wawili kutokana na mafuriko hayo.

Waswahili wana msemo 'Ukistaajabu ya Mussa, utayaona ya Firauni. Huko Kigamboni, katika kitongoji cha Mji Mwema, mvua nako imefanya mambo yake.

> **Polisi nao, mbali na tahadhari za usalama kwa umma, imetangaza vifo vya watu wawili kutokana na mafuriko hayo.**



**SAFARI YA MJIMWEMA**

Nilifahamishwa, kuwapo mafuriko yaliyoteka mazingira ya makazi mapya, watu wanashindwa kukaa katika makazi yao. Haraka nikaingia makubaliano na mwenyeji wangu, ambaye hatujawahi kukutana, anipeleke kwenye ushuhuda nyumbani kwake.

Nikiwa nimeshafika kwa ratiba ya ahadi, namsubiri kwa wastani wa dakika tano katika kituo cha daladala, mara anawasili na kujitambulisha kwa jina la Mama Witty.

Muda huo kulikuwapo mvua zilizoendelea zilizofanya tushindwe kuendelea na safari, badala yake tukaamua kupumzika kwanza, hadi zilipoisha.

Tukaanza safari na daladala ndogo aina ya Toyota Hiace maarufu kama 'vipanya' kuelekea Mji Mwema. Muda wote huo nimerakwa na hulka ya udadisi. Mwanzo, wa safari kuelekea Mashariki, ulikuwa na ushuhuda wa maeneo yaliyotokewa na madimbwi makubwa ya maji, ambayo si mageni kwetu.

Kadri safari ilivyosonga nilizidi

# ivyofurika kona zote



kushuhudia athari za madimbwi makubwa ya maji na baada ya wastani wa dakika 25, tulishafika katika stendi yetu na kushuka.

**USHUHUDA KAMILI**

Hapo tukaanza 'kukata' mitaa nikiongozwa na mwenyeji wangu Mama Witty. Ni wastani wa mwendo mdogo wastani wa mita 500, ghafla naanza kushuhudia maajabu.

Zinaibuka nyumba zinazoonekana kuelea, mithili ya zilizojengwa katikati ya bahari, ikizingatia si umbali mrefu kutoka pwani wa bahari ya Hindi. Nilishituka sana na sikuweza kuvumilia. Nilimuuliza mwenyeji wangu kwa kauli "Je watu wanaishi hapa?"

Mama Witty kwa unyonge, alinijibu akiniangalia katika uso ulibeba ishara ya masikitiko makubwa: "Ndiyo, tena nyumba yangu ile palee (akionyesha nyumba yake kwa kidole)".

Wakati nikiendelea kushangaa, ilhali naendelea na safari katika eneo hilo linalofahamika mitaa ya Ungindoni, mwenyeji wangu anavua viatu na kutembea juu ya maji huku, akiniangalia kwa huzuni, uso wake ukibeba ishara kuwa nami nivue viatu kumfuata.

Hapo, tunaanza kutembea katika maji baridi na kwa mwendo wa taratibu, kwa kuwa ndani ya maji kuna hatari ya mchanganyiko wa tope,vipande vya miti na kokoto ambazo hatuzioni .

Kutokana na kuongezeka kwa kina cha maji kadri tulivyosonga mbele , ilitulazimu kuahirisha kupita njia ile na kurudi nyuma kutafuta njia mbadala wa kufika nyumbani kwa Mama Witty.

Ilikuwa imebaki umbali wastani wa hatua 100 mbele yetu, lakini kwa mwendo taratibu, tunageuka nyuma. Mama Witty

> **Tumeshangaika sana kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili kwa kuwasiliana na viongozi mbalimbali wa serikali na tuna barua kadhaa kama ushahidi, lakini hakuna kinachofanyika, zaidi ya kupewa matumaini hewa kila siku.**



anatoa ufafanuzi wa picha halisi:

"Tumeshangaika sana kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili kwa kuwasiliana na viongozi mbalimbali wa serikali na tuna barua kadhaa kama ushahidi, lakini hakuna kinachofanyika zaidi ya kupewa matumaini hewa kila siku."

Hayo yanaendelea tukiwa katika njia mbadala ya kufikia makazi yake, ambayo tulikwama tukiwa umbali wa mita 100 tu mbele yetu.

Tukiwa tumeshika njia nyingine mbadala unaoonekana kuwa na maji kiasi si kingi sana, ilituchukua safari yenye mzunguko mrefu sana kupaona tena nyumbani kwa Mama Witty.

Nikiwa nashangaa na kuangaza huku na kule, nazishuhudia nyumba nzuri za kifahari katika eneo hilo, zikiwa katikati ya maji. Kasoro ya eneo imezitia doa kubwa makazi hayo.

Mara tunafika nyumbani kwa Mama Witty. Ni nyumba kubwa na nzuri, mwonekano bora, wote umevurugwa. Kwa mara nyingine nashindwa kuvumilia kuhoji maswali yangu ya kidadisi, natamka: "Mbona ni kama pana jaruba la mpunga hapa nje?"

Ni swali linalorejea dhana katika utangulizi wa hali ya hewa ya Dar es Salaam, pia katika mitaa ya Ungindoni , wilaya ya Kigamboni, mtu anaweza kufikiri watu wamejenga katikati ya bahari.

Mama Witty ananifafanulia kuwa umbile la jaluba, linatokana na eneo ambako kulikuwapo ukuta ambao ni mwendelezo wa Jengo Lake, sasa imekuwa kingo na kuikusanya maji kwa mtindo wake.

Tukiwa nje ya nyumba yake, ananieleza mafuriko ya ndani yalivyo, sebuleni ndiko kulikojaa maji zaidi na wakalazimika kukusanya vitu vyote katika chumba kimojawapo chenye unafuu wa mafuriko, kama ilivyo vyumba vingine.

Mtazamo huo ndio namna iliyotawala eneo zima la Ugindoni, Mjimwema. Hivi sasa nyumba zote zimo katikati ya maji.

Ni maeneo ya makazi ambayo watoto walizoea kucheza kwa madaha, sasa yamegeuka majaluba. Mvua imewaletea taharuki kubwa.

**SAUTI ZA WAKAZI**

Mkazi wa kata ya Ungindoni, anayejitambulisha kwa jina moja, Rioba, anasema wamekuwa wakipata tabu ya katika makazi yao nyakati za mvua, licha ya kutafuta ufumbuzi wake kwa muda mrefu, pasipo mafanikio.

Analalamika kwamba, wamekuwa wakipatiwa ahadi zisizotekelezeka kutoka kwa waliowatambulisha kuwa ni 'viongozi wao.'

"Tumeshangaika sana kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili kwa kuwasiliana na viongozi mbalimbali wa serikali na tuna barua kadhaa kama ushahidi, lakini hakuna kinachofanyika, zaidi ya kupewa matumaini hewa kila siku," anasema.

"Awali nilifikiri kuwa eneo hilo ni kati ya maeneo yaliyopo bondeni, hivyo kutokuwa na uhalali wa kuishi. Lakini nilipouliza, nikaelezwa kuwa eneo hilo ni halali watu kuishi, kwa kuwa limepimwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

"Hapa lina miaka hata 20 na linajulikana na viongozi wote. Kila anayekuja, anaangalia tu na kupaacha hivyo hivyo. 'Ma - DC,'mbunge, mkurugenzi ( wa Halmashauri) wote wanalijua tatizo hili," anasema Rioba.

**MWENYEKITI WAO**

Mama Witty anasema, kutokana na kujaa kwa maji katika makazi yao, wenzake walimchagua kuwa mwenyekiti wa kutafuta ufumbuzi katika mamlaka za serikali, lakini bado juhudi zake hazijazaa matunda.

Anataja baadhi ya mamlaka husika ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Kigamboni, Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni.

Kwa mujibu wa Mama Witty, baadhi ya wakazi wamefikia maamuzi ya kuyahama makazi kwa muda kila msimu wa mvua unapofika na kurejea baada ya msimu kwisha.

Kila msimu wa mvua , ni kipindi cha wanajinsia zote, kupandisha nguo juu, baadhi katika hali ya kujidhalilika, huku wamevua viatu, waweze kuyafikia makazi yao Ungindoni, Mjimwema.

AFYA

# Ilikojificha shida ya saratani ya kizazi kwa kinamama

• Inavyowahiwa umri wa usichana




Mtaalamu wa chanjo kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Lotalis Gadau, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani). **PICHA: YASMINE PROTACE.**

**Na Yasmine Protace**

IMEJULIKANA saratani ya mlango wa kizazi ni ugonjwa hatari unaochangia vifo kwa wanawake wengi nchini.

Kitaalamu, inaelezwa virusi aina ya papiloma vinavyosababisha aina hiyo ya saratani, vinaambukizwa kwa njia ya tendo la ndoa kutoka kwa mtu mwenye virusi hivyo, pindi asipotukia kinga husika.

Nchini Tanzania, chanjo dhidi ya saratani hiyo ya mlango wa kizazi kwa sasa inatolewa kwa wasichana wenye umri wa miaka 14, kwenye maeneo yote zinakotolewa huduma za chanjo.

Ili msichana apate kinga, kamili anahitaji kupatiwa dozi mbili, ya kwanza ni pindi anapotimiza umri wa miaka 14 na dozi ya pili hutolewa miezi sita baadaye.

Mtaalamu kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa amii, Jinsia, Wazee na Watoto, Lotalis Gadau, anasema chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi, hutolewa mara mbili, ili kumhakikishia mhusika kinga kamili.

Gadau, ambaye ni mtaalamu wa chanjo kutoka wizara hiyo, anasema chanjo dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi ni haki ya kila binti mwenye umri wa miaka 14 na kuendelea.

Anaongeza kuwa, watu wengi hupoteza maisha kutokana na ugonjwa huo na ndiyo sababu inayoifanya serikali kuona haja ya kuwapo ulazima wa kuanzisha chanjo hiyo, ili kupunguza idadi ya waathirika na matukio ya vifo.

Mtaalamu huyo anasema, asilimia 70 wagonjwa huwasili katika vituo husika wakiwa katika hatua za mwisho na inachangia wengi kufa.

Gadau anasema, pia katika kundi lote la saratani zinazogundulika, aina hiyo ya mlango wa kizazi imekuwa ikishika nafasi kubwa katika kuleta mauti, kinamama wengi wakiwa waathirika.

Anatoa takwimu kwamba, kuna wastani wa watu 100,000 wanaofika kufanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi, kati yao watu 34 hugundulika kuwa na maambukizi hayo.

Anasema kuwa, saratani ya mlango wa kizazi inaongoza kwa ukubwa wa tatizo nchini.

Mtaalamu huyo anasema, serikali imeweka mikakati ya kuwakinga wasichana kwa gharama ya Sh. 30,000 kwa dozi ya kwanza.

Pia, anatumia fursa ya kuwaelimisha mabinti haja ya kubadili tabia ya kuendekeza tabia zinazotoa fursa ya kuendekeza magonjwa ya kuambukizana, kwa njia ya kujamiiana.

Anasema katika wakati wa chanjo, huwa unafanyika uchunguzi wa awali, kubaini kama kuna namna yoyote ya maambukizi.

Wito wake kwa jamii ni kwamba ijitokeze katika vituo vya afya kuchunguza afya zao, ili wajitambuea ama wameambukizwa au la na kupata matibabu.

Gadau anasema kuwa walipoanzisha chanjo kwa mabinti, walitarajia kuwafikia watoto 600,000, lakini hawakufanikiwa kutokana na baadhi ya wazazi kuwa na uelewa duni wa azma, pia kinachoendelea kufanyika. Kumekuwapo madai ya hofu za wazazi, kwamba upimaji afya za watoto na hatua za kuwakinga, kunachangia mtoto kokosa uzazi ukubwani, jambo ambalo mtalaamu huyo analipinga.

Analiainisha hilo kuwa ni imani potofu dhidi ya chanjo na dai hilo halina ukweli wa aina yoyote, akisisitiza kwamba usahihi ni kutokuwapo madhara ya aina yoyote kwa msichana husika.

Gadau anafafanua ukweli ambao ni kinyume na madhara tajwa, kwamba mtu anapopata chanjo, inakuwa mkombozi kwake kumlinda na kumkinga na magonjwa kupitia chanjo tajwa.

## Kuendekeza mila kunavyowabebesha mimba wanafunzi wilayani Kishapu

INATOKA UK.17

**MWANAHARAKATI**

Clement Benard, ni mwanaume aliyejengewa uwezo na Shirika la Save the Children katika harakati kutokomeza mila na desturi zilizopitwa na wakati na watakuwa wakiyaendesha kwa kukusanya wanaume kwenye kata mbalimbali wilayani humo na kutoa elimu kupitia midahalo na mikutano.

Anataja elimu ni kwa wazazi kuachishwa tabia ya kukumbatia tabia ya kuwaficha watuhumiwa na kutokwenda mahakamani kutoa ushahidi, mwelekeo unaosaidia kukomesha tabia hasi.

**HAKIMU**

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo wilayani Kishapu, Athumani Katundu, anasema uendeshaji kesi zinazohusu ujauzito wa mwanafunzi ni ngumu, kwani wahusika wengi humaliza kesi hizo ‘kimya kimya’ na hatimaye wanajiengua kwa kutohudhuria mahakamani kutoa ushahidi, hata kesi kufutwa.

Rai ya hakimu huyo, ni kwamba jamii inapaswa kupewa elimu ya madhara wanafunzi kupewa ujauzito au kuolewa katika umri mdogo na kuacha tabia ya kumaliza kesi kimya kimya, ndiyo majibu ya utokomezaji



Wanawake wa Kishapu kwenye tamasha la Mwanaume Jasiri, linalopinga mimba na ndoa za utotoni kwa mabinti. **NA MPIGAPICHA WETU**



## Ubalozi Marekani wahamasisha wanafunzi kujifunza Kiingereza

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UBALOZI wa Marekani nchini kwa kushirikiana na Kituo cha Redio cha Kijamii cha Highlands Fm, umezindua programu maalum ya kuwahawamasisha wanafunzi wa shule za msingi zilizopo jijini Mbeya kujifunza na kuzungumza lugha ya Kingereza.

Wakizungumza juzi na waandishi wa habari kwenye uzinduzi huo, Ubalozi wa Marekani ukiongozwa na George Chinnery, ulisema lengo ni kuhakikisha wanafunzi wa Kitanzania wanahamasika na kupenda kujifunza na kuongea lugha ya Kiingereza.

Chinnery alisema programu hiyo ambayo inaitwa (lets speak), itahusisha shule mbalimbali za msingi zenye mchepuo wa Kiingereza ambazo ni Azimio, Sisimba na St. Marys.

"Tumeamua kuanzisha programu hii kwenye shule za msingi ili kuwawezesha watoto wetu kuendana na ushindani wa soko la ajira sababu ya kukua kwa teknolojia, kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kumuandaa mtoto kuanzia akiwa mdogo ili waweze kukabiliana na mazingira ya aina yoyote hata anapokuwa mtu mzima," alisema Chinnery.

Kwenye uzinduzi huo, wanafunzi walipata nafasi ya kujadili pamoja na kujibu maswali yanayohusu lugha ya Kiingereza na washindi walipatiwa zawadi ya redio na nyenzo za kujifunzia.

Mkurugenzi wa Kituo Cha Redio cha Jamii cha Highlands, Jacqueline Mwakyambiki, alisema programu hiyo itakuwa ni endelevu na kwamba waliomba ufadhili kutoka ubalozi wa Marekani baada ya kutambua kuna changamoto ya lugha ya Kiingereza kwenye shule za msingi hususani za serikali.

Alisema programu hiyo itahusisha mijadala, maigizo, maswali na mbinu nyingine za ufundishaji ili kuwajengea uelewa wanafunzi namna ya kuzungumza lugha hiyo.

"Kwa kushirikiana na walimu pamoja na wadau tutafanya tathmini ili kufahamu kama programu yetu imeleta tija kama tulivyokusudia kwa sababu lengo letu ni kuona watoto wanapenda kuzungumza lugha ya Kiingereza.

Naye mwakilishi kutoka ofisi ya Ofisa Elimu jijini Mbeya, Christina Mwakyusa, alisema shule za msingi jijini humo zinakabiliwa na changamoto kubwa ya watoto kushindwa kuzungumza na kuandika lugha ya Kiingereza.

# TCRA yazindua usajili laini za simu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imezindua usajili wa laini za simu kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) utakaosaidia kuondoa mianya ya uhalifu inayofanywa kwa njia ya mtandao.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Kanda Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Nyanda za Juu Kusini Mhandisi, Asajile John, alisema mfumo huo utawawezesha wananchi kuwa na mawasiliano bora na kudhibiti vitendo vya uhalifu.

Mhandisi John alisema mfumo huo wa kusajili laini kwa kutumia vitambulisho vya taifa ambao umeingia mkataba na TCRA utawasogeza wateja kuwa karibu na mamlaka hizo na utasaidia kuwabaini na kuwakamata wahalifu mtandaoni.

"Ili kufanikisha zoezi hili Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kusajili laini kwa kutumia vitambulisho vya taifa na kwamba mfumo huo utasaidia kuwabaini wahalifu, lakini kuweka karibu wadau na watumiaji wa bidhaa za mawasiliano," alisema Mhandisi John.

Akizindua usajili huo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, aliwasisitiza wananchi kutumia mfumo huo kusajili laini zao za simu na kwamba muda uliotolewa na serikali unatosha kuhakikisha kila mmoja anasajili laini yake kwa kutumia kitambulisho cha taifa.

Ofisa Usajili Mkoa wa Mbeya kutoka Nida, Lavia Maikontalima, alisema wananchi walilipokea agizo la serikali kusajili laini zao za simu kwa kutumia vitambulisho vya taifa na kwamba usajili huo utafanikiwa kwa asilimia 100 kwa sababu muda wa kusajili ulioongezwa.



Kinamama wachuuzi wa samaki waliokaushwa aina ya Kambale, wakisaka wateja katika eneo la Tabata Matumbi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wafanyabiashara waishauri TRA utozaji kodi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYABIASHARA jijini Mbeya, wameiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuweka mazingira rafiki ya ukusanyaji wa kodi kwa kutoza kodi zinazoendana na hali halisi ya biashara badala ya kutumia makadirio ambayo wakati mwingine hayana uhalisia.

Wito huo ulitolewa jana na wafanyabiashara jijini Mbeya, baada ya kutembelewa na maofisa wa TRA kutoka Makao Makuu na wa Mkoa wa Mbeya, waliokuwa na lengo la kubaini changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwa ni maadhimisho ya wiki ya elimu kwa mlipakodi. Mmoja wa wafanyabiashara hao, Rudiana Machemba, alisema serikali imejitahidi kuboresha mazingira ya ulipaji wa kodi na kuondoa baadhi ya tozo ambazo zilikuwa zinawakandamiza, lakini bado wanakabiliwa na changamoto ya makadirio makubwa ya kodi.


Rudiana aliiomba TRA kutengeneza mazingira rafiki ya ukusanyaji wa kodi wenye kuzingatia hali halisi ili kodi stahiki zikusanywe kwa wakati kwa ajili ya kufanya shughuli za maendeleo.

"Siku hizi wafanyabiashara tumekuwa wazalendo sana tunajitahidi kulipa kodi pamoja na kufuata miongozo mingine ya mamlaka hiyo, lakini changamoto ni makadirio ya mapato makubwa ukilinganisha na mitaji pamoja na biashara zetu," alisema Rudiana.

Paulina Peter alisema katika maadhimisho ya wiki hiyo maofisa wa TRA wazifanyie kazi changamoto mbalimbali ambazo zimeelezwa na wafanyabiashara.

Msaidizi maalum wa Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Salum, alisema katika maadhimisho hayo wanatembelea maeneo mbalimbali ya wafanyabiashara za kuzungumza nao ili kubaini kero zinazowakabili.

Alisema walisikiliza kero mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara na kuahidi kuzishughulika ikiwamo kuwatengenezea mazingira rafiki ya kufanya shughuli zao ikiwamo kurekebisha baadhi ya kasoro kwenye makadirio ya mapato.





# Vitambulisho vyazalisha mabilioni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), Selemani Jafo, amesema Sh. bilioni 20.3 zimeingizwa kwenye mfumo wa malipo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) baada ya kugawa vitambulisho vya wajasiriamali 1,022,178.

Jafo alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizungumza na Wakuu wa Mikoa kabla ya kupitia tathmini ya ugawaji wa vitambulisho hivyo, katika kikao kilichofanyika jijini hapa.

Jafo alisema ugawaji wa vitambulisho hivyo wakuu hao wameweza kuchangia upatikanaji wa Sh. bilioni 20.44 ambapo Sh. bilioni 20.3 ndizo zilizoingizwa kwenye mfumo wa TRA.

Hata hivyo, alisema takribani Sh. milioni 135.6 hazijaingizwa, na zipo mikononi mwa wakusanyaji.

Jafo alisema hadi Aprili 30, mwaka huu kiasi cha Sh. milioni 942.47 zilikuwa haijaingia kwenye mfumo wa mapato wa TRA, lakini ndani ya siku chache wakuu wa mikoa wameweza kuzifikisha kwenye mfumo fedha nyingi zaidi.

"Endapo fedha zinazokusanywa kutokana na vitambulisho vya wajasiriamali hazitaingia kwenye mfumo wa mapato wa TRA, basi fedha hizo zinakuwa mbichi na kuna hatari ya kuwapo upotevu au kutumika katika matumizi yasiyopangwa," alisema.

Aliwahimiza wakuu hao na watendaji wao ambao wamekusanya fedha za vitambulisho vya wajasiriamali kuziingiza kwenye mfumo wa malipo wa TRA mara moja.

"Nyie wakuu wa mikoa hakikisheni azma ya Rais John Magufuli ya kutaka wafanyabiashara wadogo watambuliwe na kuwaondolewa usumbufu wanapofanya biashara zao na kushiriki katika uchumi wa nchi inatimia kwa kuwaelimisha faida ya kuwa na vitambulisho," alisema.

Jafo aliipongeza mikoa ambayo imefanya vizuri katika ugawaji wa vitambulisho hivyo ambayo ni Dar es Salaam iliyogawa vitambulisho kwa asilimia 95.2. Tabora (94.58%), Kilimanjaro (79.05%), Pwani kwa (77.66%) na Tanga (72%).

Mikoa iliyofanya vibaya ni Katavi kwa asilimia 5.96, Njombe (11.14%), Rukwa (25.03%), Iringa (30.74%) na Lindi (33.58%).

Mkuu wa mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, alisema utaratibu wa kutoa vitambulisho hivyo ulikuwa mgumu hasa kutokana na wananchi kudhani kuwa serikali inatumia vitambulisho hivyo kuwalipisha kodi.

"Ukweli ulikuwa ni kuwa kiasi cha Sh. 20,000 ni cha kugharamia uchapishaji wa vitambulisho, lakini wengi waliona kuwa ni njia ya kuwalipisha kodi, lakini tuliweza kufanikiwa kwa kiasi hicho kwa kuwashirikisha viongozi wa kimila, dini na watendaji kuanzia ngazi ya kitongoji, na tukaitisha mikutano ya adhara ya kutoa elimu, na baada ya hapo mwitiko wa wananchi ukawa mkubwa," alisema.

# Waliopisha ujenzi wa uzio Ikulu walia fidia

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

BAADHI ya wakazi wa Chamwino Ikulu waliopisha ujenzi wa uzio wa Ikulu, wamelalamikia kupunjwa fidia kinyume cha makubaliano ya awali.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, walisema utaratibu unaotumika katika utoaji wa malipo ya fidia kwa ajili ya kupisha ujenzi wa Ikulu una kasoro pamoja na kutokuwa na uwazi.

Aloyce James, alisema awali katika makubaliano kabla ya kupisha upanuzi wa ujenzi huo, walikubaliana watalipwa fedha kwa ajili ya pango kwa miaka mitatu, fidia ya mali za kilimo katika eneo pamoja na fidia kwa ajili ya usumbufu.

Alisema cha kushangaza shughuli ambazo hivi sasa zipo chini ya Wakala ya Majengo (TBA) pamoja na Ofisi ya serikali ya kijiji cha Chamwino zimekuwa likiendeshwa kinyume cha utaratibu ulioelezwa awali. Alisema malipo hayo yamekuwa yakifanywa kwa uonevu kwa mmiliki wa eneo kupatiwa hundi ya fedha ambazo hatambui mchanganuo wake, hivyo kusababisha wengine kugomea malipo hayo.

"Mimi nina kiwanja pamoja na nyumba, leo hii napatiwa hundi ambayo imeandikwa Sh. milioni tatu sasa kweli Sh. milioni tatu naipelekwa wapi na hivi sasa viwanja vimepanda bei baada ya kuja kwa hii Ikulu, hiyo wanayonipa haisaidii kitu," alisema.

Alifafanua wamekuwa wakihoji kwanini malipo hayo wanalipwa bila kufanya mchanganuo, lakini wanajibiwa kuwa kama hawataki kupokea hundi hizo basi watakosa hata kiasi hicho wanachodai ni kidogo.

"Mimi nilihoji kwanini napatiwa kiasi hicho cha milioni 3, wakati nina kiwanja chenye miti na nyumba, nikaambiwa kuwa kama sitaki kutia saini kwenye hiyo hundi basi nitakosa na hizo, sasa tunaiomba serikali ije iangalie hili zoezi kwa kuwa tunatishiwa sana," alisema. Aliongeza kuwa pamoja na kulipwa kiasi kidogo cha fedha, lakini wamekuwa wakizuiliwa kuchukua kitu chochote ikiwamo matofali pamoja na mabati.

Alisema wanaiomba serikali kwenda katika kijiji hicho kujionea hali hiyo kwa kuwa wanaogopa kuwekwa ndani kutokana na namna viongozi wao wamekuwa wakiwatisha.

Akijibu malalamiko hayo kwa njia ya simu, Mkuu wa Wilaya cha Chamwino, Vumilia Nyamoga, alisema hajapata malalamiko ya watu kugomea malipo.

"Malalamiko hayo sijayapata, lakini ninachofahamu ni kwamba kila mtu kafanyiwa tathmini kulingana na utaratibu, ila watu wamekuwa wakitaka kubeba vitu ambavyo wameshafanyiwa tathmini kwa kuwa mtu huwezi kubeba mabati wakati tulishalipwa, utakuwa umejilipa mara mbili," alifafanua Nyamoga.



Watoa nasaha kutoka Shirika la Tanzania Health Promotion Support (THPS), Devotha Munna (kulia) na Anastazia Materrin (katikati), wakitoa huduma ya ushauri wa kiafya na kupima virusi vya Ukimwi kwenye banda lao, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani, yaliyofanyika, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbarawa atilia shaka uadilifu wa wahandisi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amesema wahandisi wengi nchini si waadilifu kutokana na kujihusisha na vitendo vya 'upigaji dili'.

Prof. Mbarawa aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wanafunzi wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Saalam (DIT) waliofanya ziara ya kujifunza kupitia miradi inayotekelezwa na serikali mkoani Tabora.

Alisema wahandisi wengi nchini wamekuwa wakikosa uadilifu na kusababisha miradi mingi ya maji kuwa na gharama mara mbili ya gharama halisi. Alisema wahandisi wote katika ngazi za halmashauri, mikoa hadi wizarani, wamekuwa wakifanya kazi kwa maslahi yao binafsi na siyo taifa kutokana kufanya wizi wa fedha za miradi kwa kuongeza gharama za miradi.

"Wahandisi wamekuwa wakiongeza gharama za miradi hata mara mbili ya gharama halisi, mfano mradi wa Sh. bilioni 2.7 utakuta umekuwa Sh. bilioni 4.7 na wanajipatia Sh. bilioni mbili nzima," alisema.


Prof. Mbarawa aliwataka wanafunzi hao watakapomaliza masomo yao kwenda kuwa waadilifu ili kufanya kazi kwa maslahi ya taifa.

Alisema dunia ya sasa inataka watu wanaofaulu vizuri ili kushindana na kufanya vizuri katika fani mbalimbali.

Prof. Mbarawa aliwaomba wahadhiri wa chuo hicho kuwatafutia fursa za kutembelea maeneo mengine muhimu kama ujenzi wa gati la bandari Mtwara, ujenzi wa reli ya kati ya kisasa (SRG) na maeneo mengine ili kupata mafunzo kwa vitendo kama walivyofanya kutembelea mradi wa usambazaji maji Tabora.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wa DIT, Machage Mwema, alisema wanaomba zitakapoanza ajira za Mamlaka ya Maji Vijijini (RUWASA) wao wapatiwe kipaumbele.

Alisema chuo chao ni kiwanda mama kwa kuwa kinazalisha wahandisi ambao ndio watakaoijenga Tanzania ya viwanda.





Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Ali Karume (kulia), akijadiliana jambo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Said Hassan Said, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yafafanua malipo ya kima cha chini mshahara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Haroub Ali Suleiman, amesema kuwa hakuna taasisi yoyote ya umma iliyoruhusiwa kulipa mshahara wa chini ya kima cha chini kilichowekwa na Serikali.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid, aliyetaka kujua ni lini Serikali itazisimamia taasisi za serikali ambazo zinaendelea kuwalipa watumishi na kutokuwapa mikataba ya kazi watumishi wake.

Waziri huyo alisema wizara yake imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa uamuzi huo kwa taasisi wala hakuna mtumishi aliyelalamika kulipa mshahara chini ya kima cha chini kilichoamuliwa na serikali.

Waziri huyo alitaka mwakilishi huyo kama anayo kesi kuhusiana na watumishi wa serikali kutolipwa kima cha chini cha Sh. 300,000 kilichotangazwa na Serikali asisite kuiwasilisha wizarani kwake ili aweze kuifanyia kazi na kumhakikisha kwamba agizo la serikali linatekelezwa ipasavyo.

"Hakuna taasisi hata moja katika utumishi wa umma inayolipa mshahara chini ya kima cha chini cha mshahara," alisema Waziri huyo. Aidha, alisema watumishi wote wa umma wakati wa kuajiriwa wanajazishwa mikataba.

Alieleza ni kosa kwa mtumishi wa umma kutengenezewa malipo ya mshahara katika utumishi wa umma bila kwanza kujaza mkataba wa ajira.

# Wazanzibari waelezwa kuchangamkia fursa EAC

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imewataka Wazanzibari ikiwamo wafanyabiashara kuchangamkia fursa za ajira na kiuchumi zilizopo katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) ambazo hazijatumika kikamilifu.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Ussi Gavu, wakati akijibu hoja za wajumbe waliochangia hotuba ya bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Gavu alisema soko la ajira za walimu wa Kiswahili lipo kubwa kufuatia kuwapo kwa mahitaji kwa nchi za Burundi na Sudan Kusini.

Alisema Zanzibar inayonafasi kubwa kulitumia soko hilo kwa kutoa walimu kwa ajili ya kufundisha lugha ya Kiswahili.

"Wazanzibari tuchangamkieni fursa za ajira za walimu ziliopo katika nchi za Afrika ya Mashariki....tunao walimu wengi wenye uwezo wa kusomesha lugha ya Kiswahili katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki," alisema Waziri Gavu.

Aidha, alizitaja fursa nyengine za kiuchumi ambazo wafanyabiashara kutoka Zanzibar wanaweza kuzitumia katika soko la Afrika ya mashariki.

Alisema wafanyabiashara kutoka Zanzibar ikiwamo wajasiriamali wanaweza kuonyesha bidhaa zao za kazi ya mikono kwa kutumia maonyesho ya biashara yanayofanyika katika nchi hizo.

Gavu aliwataka wafanyabiashara hao kuzalisha bidhaa zenye viwango zitakazofanikiwa kupenya katika soko la Afrika Mashariki na kuwavutia wateja.

Aliwataka kwanza kabla ya kusafirisha bidhaa zao kuzifanyia uhakiki kupitia Shirika la Viwango la Zanzibar (ZBS) ambalo litatoa cheti cha ithibati baada ya kukaguliwa.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliipitisha bajeti hiyo ya makadirio na mapato ya jumla ya Sh. bilioni 11,726.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka 2019/2020.

# Adai upinzani hauiwezi CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI asiye na Wizara Maalum wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Juma Ali Khatib, amesema kuwa sio jambo rahisi kwa vyama vya upinzani kukiondoa madarakani Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho kimefanikiwa kutekeleza ahadi zake kwa wananchi katika utekelezaji wa ilani yake ya uchaguzi.

Aliyasema hayo wakati akichangia makadirio ya bajeti ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Khatib alisema CCM imejiimarisha na kufanikiwa kwa kiwango kikubwa kutekeleza malengo ya wananchi, ambayo yametangazwa katika ilani ya uchaguzi ya chama hicho pamoja na ahadi za viongozi. Alisema vyama vya upinzani vitachukua muda mrefu kupambana na kuiondoa CCM ambayo imejiegemesha kwa wananchi ambao ndiyo wapigakura.

''CCM ni chama kikubwa, huwezi kukiondoa madarakani kirahisi kwa sababu kinafanya kazi zake kwa maslahi ya wapigakura chini ya muongozo wa ilani ya uchaguzi,'" alisema.

Khatib ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Ada Tadea, alisema katika kipindi cha miaka minane, Rais Shein amepata mafanikio makubwa ikiwamo kutekeleza ilani ya CCM katika uimarishaji wa miundombinu ya barabara. Alisema maendeleo yanayopatikana katika kipindi cha rais Shein yamekuwa yakitekelezwa katika visiwa vyote viwili vya Unguja na Pemba bila ya ubaguzi.

''Tumeshuhudia maendeleo makubwa yakifikiwa na kutekelezwa na Dk. Shein katika kipindi chake cha urais ikiwamo utiaji saini wa utafiti wa kazi za nishati ya mafuta na gesi katika visiwa vya Unguja na Pemba," alisema.

Aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kujifunza darasa la siasa kutoka kwa Rais Ali Mohamed Shein katika kujenga tabia ya uvumilivu wa kisiasa na kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

''Katika kipindi cha miaka minne nikiwa Waziri asiye na Wizara Maalum nimesoma mambo mengi ya uongozi kipindi cha Rais Shein katika kujenga uvumilivu na kuheshimu viongozi wote bila ya kujali anatoka chama kipi cha siasa," alisema.

Naye Waziri asiye na Wizara Maalum, Said Soud, aliwataka wananchi wasikubali kudanganywa kwa kuwa hakuna Serikali inayokuja madarakani kabla ya mwaka 2020. ''Tumebakiwa mwaka mmoja kuelekea katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.... wale waliokuwa wakisema Dk. Shein hatamaliza muda wake sasa sijui wanasema nini?" alihoji Soud ambaye naye anatoka chama cha upinzani cha Wakulima (AFP).

# Bil. 26.9/- kujenga barabara za Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema zaidi ya Sh. bilioni 26.9 zimetengwa kwaajili ya ujenzi wa barabara ya Jiji la Dodoma ikiwamo za mzunguko ili kujiepusha na msongamano wa magari.

Jafo alitoa kauli hiyo jana katika hafla ya utiaji saini mikataba ya utafiti na usanifu wa mifumo ya utiririshaji maji ya mvua na maji taka na mradi wa matengenezo ya miundombinu ya maji, Kata ya Hombolo, jijini hapa.

Alisema hatua hiyo imetokana na jiji hilo kukua kwa kasi tangu kutangazwa kuwa makao mkuu ya nchi.

Jafo alisema uboreshaji huo ni utekelezaji wa miradi ya uendelezaji wa miji ya kimkakati nchini ikiwamo jiji la Dodoma.

"Mradi huu unagusa takribani kilomita 70.2 na hivi sasa zaidi ya kilomita 43.92 zimekamilika tumebakisha takribani kilomita 26.7 ndio ujenzi unaoendelea," alisema.

Waziri Jafo alieleza kuwa jiji hilo ni eneo pekee litakalogusa kwa kiasi kikubwa na mitandao ya barabara.

Akizungumzia mikataba hiyo, Mkurugenzi wa jiji hilo, Godwin Kunambi, alisema miradi hiyo inatarajiwa kuanza kufanya kazi kwa kipindi cha mwaka 2020/2040.

Alisema mikataba hiyo iliyosainiwa ina thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 3.3 ambazo ni fedha za mapato ya ndani na mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema jiji hilo linazalisha maji mita za ujazo 61,000 na matumizi ya wananchi wake ni mita za ujazo 41,000, lakini mifumo ya utoaji maji ni asilimia 20.

"Hali hii inachangia kuwapo kwa tofauti kubwa ya uwiano wa uzalishaji na uondoaji maji taka jijini hapa," alisema.

Alisema sehemu kubwa ya maji taka yanaenda kwenye maeneo ambayo si sahihi.



Mbuzi wakizurura eneo la Goba jijini Dar es Salaam juzi, bila uangalizi wa mmiliki wake. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Miji 29 kunufaika mradi maji bil. 15.9/-

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Maji imesaini mkataba wenye thamani ya Sh. bilioni 15.6 na Kampuni ya WAPCOS kutoka India ili kuanza kutekeleza mradi wa maji wa miji 29 nchini.

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Profesa Kitila Mkumbo, pamoja na Meneja Mkazi wa Kampuni ya WAPCOS Ltd., Chandrasekhar Kombathula, wamesaini mkataba huo, wenye sehemu mbili, jijini Dodoma, jana.

Profesa Mkumbo akizungumza katika hafla fupi ya utiaji saini alisema kazi hiyo inafanyika ukiwa ni mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim ya India wenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani milioni 500.

Alisema mkataba uliosainiwa jana ni hatua ya awali na unahusu kazi mbili (lots) ambazo ni kuandaa taarifa ya kina kuhusu miradi yote wa miji 29 (detailed design) ikiwamo maeneo maji yatakapopatikana na ya pili ikiwa kuandaa nyaraka za zabuni ili kuwapata wakandarasi watakaotekeleza mradi.

Kampuni ya WAPCOS imetakiwa kumaliza kazi hiyo ndani ya kipindi cha miezi miwili baada ya kusaini mkataba huo jana.

"Wakandarasi wa kutekeleza mradi wanatakiwa wawe eneo la kazi ifikapo Septemba 2019. Mradi wa maji wa miji 29 unatarajia kuhudumia zaidi ya wananchi milioni mbili," ilisema taarifa iliyotolewa na kitengo cha Mawasiliano, Wizara ya Maji.

# Mkataba uwekezaji waibua mvutano kanisa, mbunge

**INATOKA UK. 9**

mmoja kati yao ni Askofu Mwakipesile.

"Nashangaa baada ya kuibuka mgogoro kuna viongozi wengine wamekuwa na madai tofauti ikiwamo kutaka kupangua mkataba kinyume na makubaliano yetu, wanataka malipo yawe na thamani ya dola moja kwa Sh. 1,500 wakati tuliandikishiana kwa dola moja kwa Sh. 1,300," alisema.

Kishimba anabainisha kuwa pia viongozi hao wamekuwa wakimlazimisha kufanya nao mazungumzo bila kuhusisha viongozi aliowekeana mkataba, jambo ambalo linamshangaza.

"Wakati mimi nawekeana nao mkataba walikuwa ni viongozi halali wa kanisa hilo, sielewi haya mambo mengine yanatoka wapi, lakini mimi nipo tayari kuwapa majengo kama watalipa fedha yangu yote iliyosalia," alisema.

**KAULI YA ASKOFU MWAKIPESILE**

Gazeti hili lilipowasiliana na Askofu Mkuu wa kanisa hilo, Mwakipesile, alijibu kwa kifupi kwamba hakuna mgogoro unaowakabili.

"Sijui kama kuna mgogoro wowote, wala sijui kuhusu huo mkataba unaoniulizia," alisema Askofu Mwakipesile.

Kwa mujibu wa barua iliyosainiwa na Katibu wa Kampuni ya Imalaseko, Ali Mkali, Januari mosi, 2018 kwenda kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa EAGT, kuanzia Desemba 2010 hadi Desemba 2017, wamefanikiwa kujirejeshea Sh. 422,204,720 kutokana na makato ya kodi.

Barua hiyo ilichanganua fedha hizo Sh. 352,744,720 ni pango la ghorofa pia Sh. 69,360,000 kwa ajili ya kodi ya godauni.

"Aidha, marejesho haya ya Tanzania Sh.422,204,720 kiasi hiki ni sehemu ya gharama zote za ujenzi wa ghorofa na jengo la ofisi ambazo ni Sh. 2,838,510,000," ilifafanuliwa katika barua hiyo ikibainisha zaidi kuwa deni lililosalia ni Sh. 2,416,305,280.

Akizungumzia suala hilo, Wakili wa Makamu Askofu Mahene kutoka Kampuni ya Giraffe Attorneys, Sylivester Sebastian, alisema hawajafanikiwa kuona mkataba wa awali wa makubaliano yaliyowekwa kati ya mwekezaji huyo na kanisa.

"Ubaya ni kwamba kutokana na mgogoro uliopo Askofu Mkuu hatoi ushirikiano unaoweza kusaidia ukweli wa mambo kuwa bayana," alisema.

"Sasa mwekezaji ameshaishi pale zaidi ya miaka mitano kwa kupitia maneno aliyoandika Katibu wake kwenye barua, ina maana anatakiwa kuwapo pale kwa miaka 47 ijayo," alisema Wakili Sebastian.

"Tunakusudia kuwapeleka wadhamini mahakamani ili watuambie mkataba huo wa awali upo wapi, pia kwa mujibu wa Sheria ya Land Registration (usajiliwa ardhi) inahitaji mkataba wowote wa kupangisha ardhi au sehemu ya ardhi usajiliwe kwa kuanzia miaka mitano kwenda mbele usajiliwe kwa msajili wa hati," alisema.

Wakili Sebastian alisema wamefuatilia ili kubaini kama mkataba umesajiliwa na wamebaini kuwa kiwanja hakina mpangaji yeyote, kwa hiyo haujawahi kusajiliwa.

"Hivyo hakuna kikwazo chochote, kama huu mkataba haupo kihalali," alisema.

## HABARI KIMATAIFA

## Wanajeshi, waandamanaji wafikia muafaka

**KHARTOUM,** Sudan

VIONGOZI wa kijeshi na waandamanaji nchini Sudan wamekubaliana kuunda serikali ya mpito, itakayokuwa madarakani kwa muda wa miaka mitatu.

Pia wamekubaliana kuwa baada ya kipindi hicho madaraka yatakabidhiwa kikamilifu ka uongozi wa kiraia.

Makubaliano hayo yamefikiwa baada ya mazungumzo yaliyoanza mwishoni mwa wiki iliyopita kuonekana kuzaa matunda, kutokana na waandamanaji kuendelea kushinikiza kuwa wanataka jeshi liachie madaraka.

Jeshi kupitia Jenerali Yasser al-Atta, limesema kuwa makubaliano hayo yatatiwa saini na pande zote mbili ndani ya saa 24 zijazo ili kuanza kutekelezwa.

Aidha, amewahakikishia wananchi wa Sudan kuwa makubaliano hayo yatatekelezwa kikamilifu ili kufikia matamanio ya raia wa taifa hilo.

Miongoni mwa makubaliano yaliyoafikiwa ni pamoja na bunge kuwa na wabunge 300 huku asilimia 67 wakitoka kwenye vuguvugu la waandamanaji, linalofahamika kama Alliance for Freedom and Change.

Maelfu ya waandamanaji kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa wameendelea kupiga kambi nje ya makao makuu ya jeshi, hata baada ya kuondoka madarakani kwa rais wa zamani Omar Al Bashir, wakishinikiza ni lazima wanajeshi waache kutawala. **RFI**

## Rais akubali kufanya kazi na upinzani

**JUBA,** Sudan kusini

RAIS wa Sudan Kusini, Salva Kiir amesema atatumia rasilimali zote zilizo kwenye mhimili wake kuleta amani na uthabiti na alitoa wito kwa vyama vyote kufanya kazi pamoja, kurejesha amani na kuruhusu watu kutembea huru.

Rais Kiir aliwasihi wabunge na maofisa wengine kuunga mkono utekelezaji wa mkataba wa kurejesha amani nchini humo ambao ulitiwa saini mwaka 2018. Katika matamshi yake siku ya Jumanne, Rais Kiir alieleza kwamba atatumia rasilimali zote zilizo kwenye mhimili wake kuleta amani na uthabiti.

Wakati wa kufunguliwa tena bunge la muda la kitaifa la Sudan Kusini mjini Juba, Rais Kiir alionya kwamba nchi haitasonga mbele hadi serikali na upinzani waweke kipaumbele utekelezaji wa mkataba huo.

Alitoa wito kwa vyama vyote kufanya kazi pamoja kurejesha amani na kuruhusu watu kutembea huru kwenye maeneo.

Rais Kiir alipongezwa na wabunge, wanadiplomasia na maafisa wengine waliokuwepo wakati aliposema kwamba yupo tayari kufanya kazi na makundi ya upinzani kurejesha uthabiti wa Sudan Kusini. **VOA**

# Namna ya kuwa salama unapotumia whatsApp

**LONDON,** Uingereza

TAARIFA kwamba WhatsApp inaweza kudukuliwa sio jambo ambalo mtumiaji yeyote wa mtandao huo wa kijamii anataka kusikia wala kuona katika kichwa cha habari.

Mtandao huo umekuwa maarufu duniani kote hususani katika nyanja ya mawasiliano.

WhatsApp kwa sasa imekuwa ikipendwa na idadi kubwa ya watu duniani kutokana na urahisi wake katika nyanja ya mawasiliano ya picha, video, sauti na ujumbe mfupi wa maneno (SMS).

**WhatsApp kwa sasa imekuwa ikipendwa na idadi kubwa ya watu duniani kutokana na urahisi wake katika nyanja ya mawasiliano ya picha, video, sauti na ujumbe mfupi wa maneno (SMS).**

Siku za hivi karibuni wamiliki wa mtandao huo ambao ndiyo wanaomiliki mtandao wa kijamii wa Facebook walieleza kuwa wadukuzi waliweza kuingilia mtandao huo na kuchukua taarifa za baadhi ya watu waliokuwa wanawahitaji.

Baada ya tukio hilo, wamiliki hao wateja wao wanaotumia mtandao huo kote duniani kuzingatia yafuatayo pindi wanapotumia mtandao huo ili wawe salama na taarifa zao.

Kwanza, wamewataka watumiaji wa mtandao huo kuimarisha 'updates' mara kwa mara, kwa sababu kwa kufanya hivyo mtumiaji atakuwa ameimarisha kinga kwa simu yake.

Pili, wanasema licha ya kwamba mawasiliano yanalindwa katika WhatsApp, wamewataka wateja wao kuepuka kuhifadhi taarifa zako kwenye anga la mtandao kama Google Drive au iCloud, kwa maana sehemu hizo siyo salama kabisa.

"Anga hilo la mtandao halina usalama kwa hivyo mtu yoyote anaweza kuingia na kuyafikia mawasilinao yako yote, iwapo unajali faragha, basi hilo ni jambo ambalo unapaswa kufikiria kuacha kulifanya" ilieleza taarifa hiyo.

Wanasema endapo ukapata ujumbe unaokuhitaji kuhifadhi mawasiliano yako, iwapo unataka kulibadili hilo unapaswa kwenda kwenye eneo la kuhifadhi chati zako yaani 'Chat Backup' inayopatika katika settings.

Kadhalika, wanasema kuna programu zaidi za kuimarisha ulinzi, uthibitisho wa mara mbili (2FA) kabla kuingia kwenye mtandao huo ambao ni njia nzuri ya kuweka taarifa salama.

Wanasema mtumiaji wa WhatsApp atatakiwa kuingiza jina lake na 'Password' baada ya hapo atahitajika kuweka alama za vidole au sauti au namba maalum zitakazotumwa na programu kwenye simu ambazo atazitumia kufungua na kuingia kwenye akaunti yake na nyinginezo za kijamii.

Siku ya Jumatatu, WhatsApp ilipendekeza wateja zaidi ya bilioni 1.5 duniani wanaotumia mtandao huo waimarishe programmu hiyo baada ya kusambaza mfumo huo mpya ulionuiwa kulinda vifaa vinavyotumia mtandao huo dhidi ya udukuzi. **BBC**



Waandamanaji Sudani wakishangilia baada ya makubaliano kufikiwa baina yao na Jeshi la kuundwa kwa serikali ya mpito itakayoongoza kwa miaka mitatu, kisha madaraka kukabidhiwa kwa wananchi. **PICHA: REUTERS**

# Marekani imesema haitaki vita na Iran

**WASHINGTON,** Marekani

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, amesema nchi yake haitaki vita na Iran, lakini ameapa wataendelea kuishinikiza Iran.

Kauli hiyo ameitoa wakati akituliza hofu ya jumuiya ya kimataifa kuhusu kuongezeka mvutano unaohofiwa unaweza kuzidisha mzozo kati ya Marekani na Iran.

Akizungumza katika mkutano wa pamoja na waandishi habari na Waziri wa Mambo ya Nje wa Urusi, Sergei Lavrov, katika mji wa Sochi, Urusi, Pompeo alisema Marekani haitafuti vita na Iran na kwamba imeweka bayana kwamba iwapo Iran itatishia maslahi ya nchi hiyo, basi kitisho hicho bila shaka kitajibiwa kwa njia inayoeleweka.

"Tunaitaka Iran ifanye mambo yake kama nchi ya kawaida, hilo ndilo tunaloliomba. Tumeweka shinikizo katika uongozi wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran ili kulifanikisha hilo. Kimsingi hatutafuti vita na Iran," alisema Pompeo.

Pompeo alisema kuwa jana alizungumza na Lavrov mjini Brussels, Ubelgiji pamoja na washirika wake wa Ulaya kuhusu kitisho ambacho Marekani inakiona kutoka kwa Iran.

Matamshi yake yametolewa baada ya Marekani kupeleka manowari ya kubeba ndege za kivita pamoja na ndege za mashambulizi aina ya B-52 katika eneo la Mashariki ya Kati, ingawa Rais Donald Trump amekanusha taarifa kwamba atawapeleka wanajeshi 120,000.

Mjumbe wa Marekani kwa ajili ya Iran, Brian Hook alisema Ulaya ina dhamana ya kuhakikisha kuwa eneo la Mashariki ya Kati lina amani na utulivu.

Hook alifafanua kuwa Iran imekuwa ikitishia kufanya mashambulizi, hivyo hawana budi kuchukua hatua za kujihami. **DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311**


## KUPOTELEWA KWA CHETI



**Rebeca Amos Nhyama** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye Index Namba S0462-0039, Kilichotolewa na Baraza la Mtihani Tanzania katika Shule ya Sekondari Wigehe mwaka 2011.

**Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha Polisi.**

**Taarifa ya Polisi KHM/RB/152/014**

215230201

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**QUEEN MACMILLAN SIRAKI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 985 CYY TOYOTA MARK X.** Chassis namba GRX 120-0015844. Engine namba **4GR EAA-5844.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MAG/RB/16074/2019.**

115230702

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**SHAURI LA MADAI NA 20. 20/2019**
**FUHUA PLASTIC PRODUCTION COMPANY LIMITED ....MDAI**
**DHIDI YA**
**HUSSEIN SELEMANI.........................MDAIWA**

Kwa : HUSSEIN SELEMAN
MWANZA AU POPOTE ULIPO

WITO WA SHAURI
Mahakama inakufahamisha kwamba wadai hapo juu wamefungua madai dhidi yako nakala yake inapatikana katika mahakama hii.

Shauri dhidi yako limepangwa kutajwa mnamo tarehe 17/05/2019 saa 2:30 asubuhi na unatakiwa kuwepo, au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya madai haya,

Zingatia kwamba kutofika kwako tarehe hiyo, shauri litapangwa kusikilizwa bila ya wewe kutaarifiwa tena, na maamuzi kutolewa.

Imetolewa kwa mkono wangu na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 17/04/2019.

215230402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;99/2019**

**Ombi la OMARI SAID MALEWA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HOJA SELENAN**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 18/05/2019.

115231102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA**
**SHAURI LA MADAI YA TALAKA NAMBARI 41 YA 2019**

**MDAI.....................NEEMA ROMAN KAVISHE**
**DHIDI YA**
**MDAIWA.....................BAZIRIUS JOHN KASESE**

**KWA: BAZIRIUS JOHN KASESE**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

**POPOTE PALE ULIPO**
Fahamu kwamba mdai ameleta madai yake Mahakamani dhidi yako. Madai haya yamepangwa kutajwa tarehe 20/05/2019.

Fahamu kwamba unatakiwa kuhudhuria Mahakamani wewe mwenyewe siku hiyo bila kukosa. Kutohudhuria kwako kutaifanya Mahakama hii iendelee na shauri hili bila wewe kuwepo na kulitolea uamuzi.

Imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15/05/2019.

215231002

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
15/05/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **IJUMAA tarehe 17/05/2019** kampuni ya **MEERO CONTRACTORS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MOSHI** kuelekea **LONGIDO ARUSHA** gari hilo lenye namba za usajili: **T.747 ASM/T.163 DLR**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 2.8**
   **Upana** – **mita 5.5**
   **Kimo** – **mita 4.2**
3. Njia itakayotumika **MOSHI hadi LONGIDO ARUSHA** kupitia **ARUSHA MJINI** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115230802

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
15/05/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI tarehe 18/05/2019 kampuni ya MEERO CONTRACTORS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MTO WA MBU -ARUSHA** kuelekea **MBANDE DODOMA** gari hilo lenye namba za usajili: **T.747 ASM/T.163** DLR
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 17**
   **Upana** – **mita 3.0**
   **Kimo** – **mita 4.8**
3. Njia itakayotumika **MTO WA MBU-ARUSHA hadi MBANDE DODOMA kupitia BABATI** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115230802

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**GIBBONS MLOWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 718 CZY. CHASSIS No. GYEW101478.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/3782/2018.**

115231202


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# LUIZ: ABRAMOVICH BADO ANA MAPENZI NA CHELSEA



**LONDON,** England

BEKI wa Chelsea, David Luiz, amesema kwamba mmiliki, Roman Abramovich bado ana mapenzi makubwa na klabu hiyo na kuongeza kwamba amefanya mazungumzo na raia huyo wa Urusi kuhusu kuongeza mkataba wake.

Abramovich amekosekana katika dimba la Stamford Bridge kwa msimu wote huu kutokana na sakata lake la mamlaka ya Serikali ya Uingereza, ambayo mwaka jana ilisitisha kuongeza muda wa Visa yake, na maafisa wa Chelsea wamelazimika kukanusha kwamba mmiliki wao ana mpango wa kuiuza klabu hiyo kwa bilionea Muingereza, Sir Jim Ratcliffe.

Na Luiz amesema Abramovich bado Chelsea ipo moyoni mwake na ameshawekeza vya kutosha.

"Amekuwa mbali na klabu, lakini moyo wake uko pale," amesema Luiz akimzungumzia Abramovich kwenye mahojiano yake na Daily Mail. "Anaipenda Klabu. Yeye ndiye aliyeijenga Chelsea.

"Kila kitu hapa Chelsea kimebadilika kwa sababu ya yeye. Matokeo yenyewe yanazungumza: mataji 15 kwa miaka 15. Alikuja hapa kufanya kitu fulani cha kuvutia na alifanya hivyo.

"Nilikuwa na nafasi ya kuzungumza naye wiki iliyopita, kuamua hatima yangu. Anaipenda klabu na kila kitu kuhusu klabu na si watu tu. Anataka kushinda kila kitu. Bado ana mapenzi makubwa na klabu na anataka kufanya mengi zaidi.

"Ni vigumu kwa upande wake, lakini moyo wake upo na sisi, anajaribu kuwa karibu na sisi kila siku. Bado ana mapenzi na klabu. Anaifikiria klabu kila wakati.

"Ana njaa kama sisi ya kufikiria kushinda mataji mengi hataki kupoteza nguvu zake bure."

# Ronaldinho azuiwa kutoka nje ya Brazil

**SAO PAULO,** Brazil

MAHAKAMA nchini Brazil, imeongeza muda wa kuendelea kuishikilia hati ya kusafiria ya mshindi wa zamani wa Kombe la Dunia, Ronaldinho na kaka yake, Assis Moreira.

Mahakama Kuu ya Brazil Jumanne ilitupilia mbali ombi la mchezaji huyo nyota wa zamani wa Barcelona na kwamba hataruhusiwa kusafiri wakati kesi yake ya jinai ya uharibifu mazingira ikiwa inaendelea.

Hata hivyo, Ronaldinho ambaye ni mchezaji bora wa mwaka wa dunia wa zamani, bado anaweza kukata rufaa.

Hati ya kusafiria ya mchezaji huyo ilizuiliwa Novemba mwaka jana kwa sababu ya kushindwa kulipa hasara ya dola milioni 2.1 katika kesi yake.

Kesi yake inahusiana na ujenzi alioufanya kwenye eneo la uvuvi na mazalisho ya samaki bila kibali katika fukwe ya mto Guaiba katika mji wa nyumbani kwao, Porto Alegre mwaka 2015.

Ronaldinho hakuwa na leseni ya mazingira ya kufanya ujenzi kwenye eneo hilo ambalo haliruhusiwi kisheria.



# Madrid kumrudisha tena Bale England




**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid, imempa 'ofa' mshambuliaji Gareth Bale kurejea Tottenham Hotspurs kwa mkopo katika usajili wa majira ya kiangazi.

Bale aliondoka Spurs kwenda Real Madrid mwaka 2013 na kuweka rekodi ya kununuliwa kwa pauni milioni 86.

Kocha Zinedine Zidane amesema klabu hiyo itamtoa kwa mkopo, lakini atavuna pauni milioni 10 na mshahara wa pauni 250,000 kwa wiki.

Spurs imetuma maombi ya kutaka kumrejesha mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Wales, baada ya kukosa mvuto kwa Zidane.

Mara kadhaa Zidane amekuwa akimtaka Bale kusaka klabu mpya ya kujiunga nayo kwa kuwa hana nafasi katika kikosi chake.

Licha ya Zidane kumuweka sokoni nyota huyo, hakuna klabu ya Ulaya iliyojitokeza kutaka huduma ya winga huyo.

Hata hivyo Gazeti la Mirror limeeleza kuwa Bale, 29, atakataa ofa ya kurudi Tottenham na hataki kuharakisha kuondoka Real Madrid, wakati huu akiwa amebakiza miaka mitatu katika mkataba wake unaomuwezesha kupokea pauni 600,000 kwa wiki.

# Solskjaer: Najua wakuijenga United

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema kumaliza vibaya kwa klabu hiyo msimu huu kumemsaidia yeye kuamua wachezaji gani anaotaka kujenga nao timu mpya.

Kiwango cha United kiliimarika mara baada ya Solskjaer kupewa mikoba ya kocha wa muda mfupi Desemba kabla ya kumpa mkataba wa kudumu na ilikuwa kwenye harakati za kumaliza kwenye nne bora katika Ligi Kuu na kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini mwisho wa msimu imeshuhudiwa timu hiyo ikimaliza ligi kwa kutoshinda mechi sita mfululizo katika mashindano yote, huku ikimaliza nafasi ya sita kwenye msimamo na kupitwa pointi 32 na mabingwa Manchester City.

Solskjaer, ambaye alipewa mkataba wa kudumu Machi mwaka huu, amebainisha kwamba klabu yake ilipoteza kiwango chake wiki za mwisho za kuelekea mwishoni mwa msimu, lakini atatumia uzoefu wake ili kuanza vizuri msimu wa 2019-20.

"Nimejifunza kwamba sipendi kupoteza," alisema akiiambia tovuti ya Manchester United. "Napenda kushinda.

"Tulianza vibaya. Vijana hawakujiamini wakati nilipokuja hapa. Tukaanza kuwa sawa. Tukashinda mechi. Kundi lote tulikuwa pamoja, na nilifurahia kushinda, lakini najua kwamba soka ni mchezo mgumu.

"Huwezi kutarajia kwamba kila kitu kitakwenda sawa kama ambavyo unavyotarajia. Tupo kwenye ligi yenye timu kubwa na ngumu na hivyo ili kufikia kwenye kiwango unahitajika kuwa fiti kwa asilimia 100."






# AGUERO: MESSI NDIYE ANASTAHILI BALLON D'OR

**MANCHESTER,** England

SERGIO Aguero, amezungumza hadharani kwamba anamuunga mkono Lionel Messi kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] na amekanusha madai kwamba anaamua kumpendelea kwa sababu ni rafiki yake wa karibu.

Awali kuliibuka sitofahamu baada ya mshambuliaji huyo wa Manchester City kuzungumza mbele ya wanahabari kwamba, mshindi ajaye wa tuzo ya Ballon d'Or anatakiwa kuwa kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Messi, mshindi mara tano wa tuzo hiyo alitolewa kwenye mchezo wa pili wa nusu fainali na Liverpool baada ya kutolewa kwa tofauti ya mabao 4-3.

Na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alimaliza nafasi ya tano kwenye orodha ya mwaka jana kwenye tuzo ya Ballon d'Or na Aguero akaandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii kuelezea kama raia mwenzake huyo wa Argentina anastahili kushinda tuzo hiyo kwa mwaka 2019.

"Huwa sipendi kufafanua kauli yangu wakati ninaponukuliwa tofauti na kile nilichokizungumza, lakini nimelazimika kufanya hivyo," alisema Aguero kupitia ukurasa wake wa Twitter.

"Nitazungumza tena. Hakuna zaidi ya Messi atakayepata kura yangu kwenye kutwaa Ballon d'Or akiwa anaendelea kucheza kama alivyofanya msimu huu."

# *Guardiola kocha bora wa msimu*

**LONDON,** England

PEP Guardiola ametajwa kuwa kocha bora wa msimu kwa mara ya pili mfululizo baada ya kuiongoza Manchester City kutetea ubingwa wa Ligi Kuu ya England.

City ilimaliza ligi kwa tofauti ya pointi moja na Liverpool baada ya kukimbizana kwa msimu mzima katika mbio za ubingwaa huo.

Ushindi mara 32 na sare mbili ziliwafanya Man City kumaliza Ligi wakiwa kileleni kwa pointi 98, tofauti ya pointi mbili kufikia 100 ambazo ilizipata msimu uliopita na pia wameshinda taji la EFL na watacheza na Watford kwenye fainali ya Kombe la FA Jumamosi.

Guardiola alitangazwa kuwa kocha bora na Chama cha Makocha wa Ligi Kuu Jumanne usiku.

"Ni heshima kupata tuzo hii," kocha huyo wa zamani wa Barcelona alisema katika ujumbe wake uliotumwa kwa njia ya video.

"Nataka kuisherehekea tuzo hii na wachezaji wangu kwa sababu wao ndio kila kitu, kwa benchi la ufundi kwa sababu tulipigana pamoja na makocha wote wa Ligi Kuu, hasa Jurgen Klopp, ambaye nilipambana naye hadi mwisho.

"Ni fahari kwetu kucheza dhidi yao wote, tulikuwa katika ushindani mkubwa dhidi yao katika mbio za kuwania ubingwa."

Kocha wa Liverpool, Klopp, Mauricio Pochettino wa Tottenhama na Nuno Espirito Santo wa Wolves wote walikuwa wakiwania tuzo hiyo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN SASA RASMI BARCA, AAGA ATLETICO

## ●●● Coutinho anukia kufunguliwa mlango wa kutokea ili kumpisha, lakini...

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann, ametangaza rasmi kuwa ataachana na klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu baada ya kuitumikia kwa kipindi cha miaka mitano.

**Mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, alisaini mkataba wa miaka mitano Juni mwaka jana, lakini mechi ya La Liga Jumamosi dhidi ya Levante itakuwa ya mwisho kwake akiwa na klabu hiyo.**

Barcelona italipa dau linalohitajika ili kuvunja mkataba wa Griezmann kiasi cha euro milioni 120 na kisha kumiliki rasmi mchezaji huyo, BBC Sport imeeleza kulitambua hilo.

"Imekuwa ni miaka mitano ya kushangaza. Asante kwa kila kitu," alisema.

"Nilitaka kuwaambia mashabiki ambao mara zote wamekuwa wakionyesha mapenzi kwamba nimechukua uamuzi wa kuondoka, kuona mambo mengine, kupata changamoto nyingine," mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, aliongeza, katika video yake aliyotupia katika mtandao wa Twitter.

"Ukweli imekuwa ni vigumu kuchukua njia hii, lakini ndicho ninahisi, ninahikitaji na ningependa kuwashukuru wote kwa mapenzi mlionionyesha katika kipindi cha miaka mitano."

Mfaransa huyo alifunga mabao 133 katika mechi 256 alizoichezea Atletico tangu alipojiunga nayo mwaka 2014 akitokea kwa majirani zao wa Hispania, Real Sociedad. Ametwaa ubingwa wa Europa League, ubingwa wa Hispania Super Cup na Uefa Super Cup katika kipindi akiwa Atletico na amekuwa mfungaji bora wa klabu hiyo katika kila kipindi kwa misimu yote mitano aliyodumu klabuni hapo.

Griezmann alikataa ofa kutoka Barcelona mwaka jana na kufungua mchakato wa mawazo yake katika waraka unaoitwa 'Uamuzi'.

Atletico pia iliishitaki Barcelona Fifa ikiituhumu kupitia mlango wa nyuma kutaka kumsajili Mfaransa huyo Desemba 2017.

Griezmann atakuwa mchezaji wa tatu wa kiwango cha juu kuondoka Atletico majira haya ya joto baada ya beki Lucas Hernandez kukubali kujiunga na Bayern Munich pamoja na mtoa huduma wao wa muda mrefu nahodha Diego Godin, aliyetangaza kuondoka wakati huu mkataba wake ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu.

### COUTINHO KUONDOKA BARCA?

Kutua kwa Griezmann Barcelona kunatoa hofu kubwa kwa mustakabali wa baadaye wa Philippe Coutinho hapo Nou Camp.

Coutinho amekuwa katika wakati mgumu wa kuhaha kurejea katika kiwango chake tangu alipojiunga na klabu hiyo akitokea Liverpool kwa pauni milioni 142 Januari mwaka jana, na chanzo kimoja kimeeleza kwamba kutua kwa Griezmann kutoka Atletico Madrid kunaweza kutoa nafasi kwa Mbrazil huyo kuondoka.

Kuna tetesi pia zinamhusisha Luis Suarez, lakini mshambuliaji huyo amekuwa na mchango mkubwa kuliko Coutinho na inaonekana kama Muuruguay huyo atabaki majira haya ya joto kabla ya kuondoka baadaye.

## ZISIKUPITE

### BAYERN YAMGEUKIA SANE

BAYERN Munich imefungua meza ya mazungumzo na Manchester City kuhusu uwezekano wa kumsajili winga Mjerumani Leroy Sane. ***(Daily Record)***

### BARCA, ATLETICO ZAKUBALIANA

RAIS wa La Liga, Javier Tebas amesema Barcelona imekubali italipa dau la kuvunja mkataba wa Antoine Griezmann kwa Atletico Madrid. ***(Cope - in Spanish)***

### MADRID YAMFUATA POGBA

REAL Madrid imefunga safari kumfuata kiungo Paul Pogba, wakati huu Manchester United ikihitaji dili hilo kufanyika kwa pauni milioni 150. ***(Independent)***

### CHELSEA YAIKOMALIA MADRID

LICHA ya taarifa kueleza kuwa Real Madrid imekubali kutoa pauni milioni 86 ili kumpata kiungo Eden Hazard, 28, Chelsea inataka pauni milioni 100. ***(Evening Standard)***

### BALE AIKATAA TOTTENHAM

MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale, 29, atakataa ofa ya kurudi Tottenham na hataki kuharakisha kuondoka Real Madrid, wakati huu akiwa amebakiza miaka mitatu katika mkataba wake unaomuwezesha kupokea pauni 600,000 kwa wiki. ***(Mirror)***

### COUTINHO SOKONI BARCELONA

BARCELONA inataka kumuuza kiungo Mbazil Philippe Coutinho, 26, majira haya ya joto, lakini haitamruhusu kuondoka chini ya euro milioni 100. ***(Sport)***

### SANCHEZ KWA MKOPO INTER

MANCHESTER United inaweza kumlipa mshambuliaji wa kimataifa wa Chile, Alexis , 30, kiasi cha pauni milioni 12 mwaka ujao ili kwenda kucheza kwa mkopo Inter Milan. ***(Mirror)***

### SESSEGNON AICHAGUA SPURS

TOTTENHAM ni chaguo la kwanza kwa beki wa Fulham, Ryan Sessegnon, kuliko Manchester United kwa sababu anataka kuendelea kubaki London na kufanya kazi chini ya Mauricio Pochettino. ***(Evening Standard)***

### MARTIAL HAUZWI UNITED

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ufaransa, Anthony Martial, 23, hatauzwa na Manchester United majira haya ya joto kwa sababu ni mmoja wa wachezaji wanaomvutia Mwenyekiti mwenza wa klabu hiyo, Joel Glazer. ***(ESPN)***

### SOUTHGATE KUMUITA KANE

GARETH Southgate atamuita mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane, 25, katika kikosi chake kitakachocheza mechi ya Ligi ya Maitaifa ya Ulaya mwezi ujao baada ya kuhakikishiwa nahodha huyo wa England atakuwa fiti kucheza Ureno. ***(Guardian)***

### YATOA MASHARTI KWA CANCELO

JUVENTUS itamuuza tu mchezaji anayewindwa na Manchester United na Manchester City, Joao Cancelo kwa masharti mawili kama itaona ofa ya takriban pauni milioni 60 inafikiwa na beki huyo wa kulia wa Ureno mwenye umri wa miaka 24, ataomba kuondoka majira haya ya joto. ***(Calciomercato)***

# ZFF yasukwa upya Mjini Magharibi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF) ngazi ya Mkoa wa Mjini Magharibi, limetaja kamati sita ambazo zitafanya kazi kwenye mkoa huo kwa lengo la kukuza na kuendeleza soka mkoani hapo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Ukumbi wa Uwanja wa Amaan, Mwenyekiti wa ZFF Mkoa wa Mjini Magharibi, Husein Ali Ahmada, alisema kamati hizo sita pamoja na waliochaguliwa kuziongoza, anaamini wanaweza kuzisimamia na kulipeleka mbali soka la Zanzibar katika ngazi ya mkoa huo.

Akizitaja kamati hizo mbele ya waandishi wa habari, alisema Kamati ya Fedha na Mipango ambayo itaiongoza yeye, Ahmada akiwa mwenyekiti na Abdurabi Mahfudhi katibu, wajumbe watakuwa ni Haji Ali, Dk. Said Seif na Haji Khmis, huku Kamati ya Ufundi na Maendeleo ya Soka Mwenyekiti akiwa ni Said Mohmed na Katibu Salum Ali Haji ambapo wajumbe watakuwa Ibrahim Mohmed na Nasra Juma.

Kwa upande wa Kamati ya Maendeleo ya Vijana na Wanawake, alisema Mwenyekiti wa kamati hiyo ni Omar Bakar na Katibu wake ni Alawi Haidar huku wajumbe wakiwa ni Othman Mohmed, Mwajuma Ali na Khatma Mwadini. Kamati ya Waamuzi, Mwenyekiti ni Juma Ali, Katibu wake ni Haji Majid na wajumbe ni Talib Haji, Mussa Hassan na Idd Shabani.

Aliitaja kamati nyingine kuwa ni ya tiba itakayoongozwa na Hamed Salum mwenyekiti na Katibu wake, Maulid Massoud ambapo wajumbe wa kamati hiyo watakuwa ni Ramadhan Makungu Nassor, Dk. Hassan Haji na Issa Juma wakati kamati ya sita ikiwa ni Soka la Ufukweni ambayo itaongozwa na Mwenyekiti Abas Khamis na Katibu wake akiwa ni Kijo Nadir huku wajumbe wakiwa ni Abdallah Thabiti 'Dula Sunday', Fahad Khamis pamoja na Omar Kilupi.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 36 | 26 | 5 | 5 | 55 | 25 | 83 |
| 2. Simba | 33 | 26 | 4 | 3 | 69 | 14 | 82 |
| 3. Azam | 36 | 19 | 12 | 5 | 50 | 21 | 69 |
| 4. Kinondoni MC | 36 | 11 | 16 | 9 | 36 | 25 | 49 |
| 5. Mtibwa Sugar | 35 | 14 | 7 | 14 | 36 | 29 | 49 |
| 6. Lipuli | 36 | 12 | 12 | 12 | 30 | 36 | 48 |
| 7.Singida United | 35 | 11 | 11 | 13 | 28 | 35 | 44 |
| 8. Ndanda | 34 | 11 | 11 | 12 | 22 | 31 | 44 |
| 9. Coastal Union | 35 | 10 | 14 | 11 | 31 | 41 | 44 |
| 10. Tanzania Prisons | 36 | 10 | 13 | 13 | 27 | 29 | 43 |
| 11. Kagera Sugar | 35 | 10 | 13 | 12 | 31 | 37 | 43 |
| 12. Mbao | 35 | 11 | 10 | 14 | 23 | 35 | 43 |
| 13. Ruvu Shooting | 36 | 10 | 12 | 14 | 33 | 41 | 42 |
| 14. Alliance | 35 | 10 | 11 | 14 | 28 | 38 | 41 |
| 15. Stand United | 35 | 11 | 8 | 16 | 33 | 44 | 41 |
| 16. Mbeya City | 34 | 12 | 7 | 15 | 35 | 36 | 43 |
| 17. Biashara United | 34 | 10 | 10 | 14 | 26 | 31 | 40 |
| 18. JKT Tanzania | 35 | 9 | 13 | 13 | 22 | 32 | 40 |
| 19. Mwadui | 35 | 10 | 7 | 18 | 38 | 48 | 37 |
| 20. African Lyon | 34 | 4 | 10 | 20 | 21 | 46 | 22 |

# WAZAMBIA KUITIBULIA SIMBA KWA KAKOLANYA

**Na Somoe Ng'itu**

SIKU chache zikiwa zimepita tangu aliyekuwa mlinda mlango namba moja wa Yanga, Beno Kakolanya, kutangazwa kuwa huru, klabu za nje ya Tanzania ndizo zimeonekana kufanya mazungumzo rasmi ya kumwania golikipa huyo.

**Kwa hapa nchini klabu zinazotajwa kumwania kipa huyo ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba na Azam FC zote za jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa golikipa huyo, Suleiman Haroub, alisema klabu moja ya Zambia (jina tunalihifadhi) imekuwa ikimhitaji Kakolanya tangu msimu uliopita, lakini ilikuwa ikisubiri amalizane na Yanga.

Haroub alisema Kakolanya atafikia uamuzi wa kusaini mkataba na klabu ambayo itakuwa tayari kulipa dau ambalo ameliweza "mezani" bila kujali timu hiyo itakuwa ya ndani au nje ya Tanzania.

"Bado mambo hayajafikia mwisho, ila klabu ambayo inaongoza katika kuwania saini ni ya Zambia, ni mapema kukutajia jina kwa sababu tulizokubaliana, hawa walianza mapema na sisi ndio tuliwasimamisha ili kumalizana kwanza na Yanga," Haroub alisema.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa mchezaji wake huyo amechelewa kusaini mkataba mpya kwa sababu anahitaji kusajiliwa na timu ambayo itaheshimu makubaliano.

Kakolanya aliamua kujiweka pembeni katika kikosi cha Yanga kutokana na uongozi wa klabu hiyo kushindwa kuwalipa wachezaji mishahara yao kwa wakati huku nyota wengine wakikacha mazoezi kwa visingizio tofauti na baadaye kurejea kundini.

Hata hivyo, kwa hapa nchini, dirisha la usajili bado halijafunguliwa mpaka Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu itakapomalizika.



Papy Tshishimbi (katikati) akipongezwa na wachezaji wenzake baada ya kuifungia Yanga bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MAKTABA**

# *Kiungo Coastal ajiweka sokoni*

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kiungo wa Coastal Union ya jijini Tanga, Adeyum Ahmed, akizikaribisha klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara kumsajili kwa ajili ya msimu ujao, nyota huyo amesema kuwa wachezaji wa timu hiyo hawastahili kupata lawama yoyote kutokana na kichapo cha aibu walichopokea kutoka kwa Simba.

Coastal Union ilifungwa mabao 8-1 na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara katika mchezo wa ligi hiyo uliochezwa wiki iliyopita kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Adeyum, alisema wachezaji waliingia uwanjani wakiwa na uchovu, kwa sababu walisafiri usiku kutoka Tanga kuja jijini ili kucheza mechi hiyo iliyokuwa ya kiporo.

Adeyum alisema uamuzi huo uliofanywa na viongozi wa klabu yao haukuwa sahihi kwa sababu wachezaji walishuka dimbani wakiwa na uchovu wa safari.

"Tuliamka saa nane usiku kuanza maandalizi ya safari, tuliingia uwanjani tukiwa na uchovu na baadhi yetu tumefunga, kwa kweli hakutuwa vema siku hiyo," alisema mchezaji huyo. Aliongeza kuwa amebakiza siku chache kabla ya mkataba wake na timu hiyo kumalizika na sasa yuko huru kufanya mazungumzo na klabu yoyote ambayo itakuwa inahitaji huduma yake.

"Coastal niliisaidia mwaka mmoja, kwa maana hiyo ligi ikimalizika tu, nami ninakuwa huru, kama watanihitaji, tutazungumza upya," aliongeza kiungo huyo wa zamani wa Kagera Sugar kutoka Zanzibar.

Coastal Union yenye pointi 44 ambayo iko chini ya Kocha Mkuu, Juma Mgunda, jana ilikuwa ugenini kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya ikikutana na wenyeji Mbeya City.

Alhamisi Mei 16, 2019
Nipashe

# Michezo



Griezmann rasmi Barca, awaaga Atletico HABARI UK.30

WANIA...



Beki wa pembeni wa Yanga, Paul Godfrey, akiwania mpira na mchezaji wa Ruvu Shooting (chini), kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Yanga ilishinda 1-0. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Aussems afunguka anapoihofia Mtibwa

●●● Asema ushindi unaweza kupatikana, awaonya wachezaji Simba kuwa watapaswa...

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kupunguzwa kasi katika mbio za ubingwa kwenye michezo miwili iliyopita, mabingwa watetezi, Simba, wanarejea dimbani kuwakaribisha Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**Mechi hiyo ni ya kiporo na timu hizo mbili zitakutana tena katika mchezo wa kufunga pazia msimu huu wa 2018/19 ambao utachezwa Mei 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.**

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, aliliambia gazeti hili kuwa anatarajia kukutana na ushindani katika mchezo huo, kwa sababu wapinzani wao hawana presha ya aina yoyote.

Aussems alisema kuwa amewataka wachezaji wake kusahau matokeo ya mechi ziliyopita, na kuangalia mchezo dhidi ya Mtibwa Sugar ambao upo mbele yao.

"Itakuwa mechi ngumu, Mtibwa Sugar ni wazuri, wana wachezaji wenye uwezo na wazoefu, lakini tunatarajia tutapata matokeo mazuri," alisema Mbelgiji huyo.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema wamejiandaa kupambana na kuonyesha kiwango cha juu kama ilivyokuwa katika mchezo uliopita.

Rweyemamu alisema wachezaji wote wako tayari kwa mchezo huo na wanajua bidii pekee ndiyo itakayowasaidia kutimiza malengo yao.

"Tutaenda kupambana, kama tulivyopambana katika mechi ya Azam, ari ya wachezaji ilikuwa juu sana, kwa kifupi nikwambie wachezaji wote wako tayari, isipokuwa Wawa (Paschal), ila naamini tutakuwa naye katika mechi za mbele ya safari," Rweyemamu alisema.

Yanga ambao wamecheza mechi 36 na wana pointi 83, ndio vinara wa ligi hiyo yenye kushirikisha timu 20 ikifuatiwa na Simba yenye pointi 82 zilizotokana na mechi 33 wakati mabingwa wa Kombe la Kagame, Azam FC wanafuatia wakiwa na pointi 69 baada ya kushuka dimbani idadi sawa ya michezo na Wanajangwani hao.

## Ajibu aona ubingwa wakiisikilizia Simba

**Na Mwandishi Wetu**

NAHODHA na mshambuliaji wa Yanga, Ibrahim Ajibu, amesema watajipanga imara kuhakikisha wanashinda mechi zao mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizobaki msimu huu, huku wakisubiri yatakayojiri katika michezo mitano ya watani zao, Simba iliyobakiza.

Yanga ilirejea kileleni juzi baada ya kuwafunga Ruvu Shooting bao 1-0 na kufikisha pointi 83 wakati mabingwa watetezi, Simba wenye pointi 82 wakashuka kwa nafasi moja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ajibu, alisema bado mpaka sasa nafasi ya kutwaa ubingwa iko wazi kati yao na Simba na hiyo itajulikana kutokana na matokeo ya mechi tatu za viporo za Simba ilizobakiza.

Ajibu alisema wao jukumu walilo nalo ni kupambana kuchukua pointi tatu katika kila mechi wanayocheza na wanaamini Mungu anaweza kuwapa furaha wanayoihitaji.

"Kwanza tunamshukuru Mungu tumepata ushindi, suala la ubingwa bado lipo kwa sababu mpaka sasa hakuna ambaye ana uhakika, tumejipanga kumaliza kwa kupata ushindi, ingawa sisi tuna mechi mbili na wenzetu Simba wana mechi tano, halafu tutaangalia yajayo," alisema mshambuliaji huyo.

Naye Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera, ambaye amekuwa haishiwi maneno, alisema jana kuwa amefurahi kupata ushindi, lakini amelalamika kikosi chake hakikupata muda wa maandalizi tangu kilipomaliza mchezo dhidi ya Biashara United.

Zahera alisema kuwa "kiafya" halikuwa jambo sahihi, lakini iliwalazimu washuke dimbani kutokana na ratiba waliyokuwa nayo.

"Tulikuwa wazito, kwa sababu tangu tunacheza Musoma hakuna mchezaji ambaye alishika mpira, hii haijawahi kutokea duniani, leo nilijua tutapata matatizo sana kwa sababu hatukujiandaa, tulipata nafasi ya kwanza tukaitumia, baadaye tukapata nafasi tatu hatukuzitumia na hii ilitupa tabu," aliongeza Zahera.

Yanga itashuka tena uwanjani Mei 22, mwaka huu kuwakaribisha Mbeya City na itamaliza msimu huu kwa kuwavaa mabingwa wa Kombe la Kagame, Azam FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >